SportPesa
TZS. 878,152,880
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**POLISI** Dar yaua watatu tuhuma za ujambazi


Watanzania tupalilie uchifu wa kisasa tu
BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Uongozi Dar wafunguka undani ubishi wa Machinga dhidi ya agizo wanndoke
JICHO LA TATU LA RAIS SAMIA;
Mbinu mkakati Utambulisho Mikoa utakavyochochea maendeleo kitaifa
• Utamaduni wa tamasha kubeba jukumu

UKURASA 11

# Nipashe

Ijumaa Januari 28, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580839
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Rais Samia ataja matukio matano katika maisha yake

UKURASA 2

'HAPPY BIRTHDAY'



Rais Samia Suluhu Hassan akikata keki kusherehekea kumbukumbu ya siku yake ya kuzaliwa Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma, jana. **PICHA: IKULU**



## Mzee miaka 80 ajinyonga hadi kufariki

UKURASA 3

UKURASA WA 4

### PM ATOA MAAGIZO 13 KUHUSU KISWAHILI



WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa maagizo 13 kwa chuo kikuu, mabalozi...

UKURASA WA 4

### LHRC YACHARUKIA MATUKIO YA MAUAJI

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimelaani matukio ya mauaji yanayoendelea kutokea maeneo mbalimbali nchini...

UKURASA WA 3



### TAKUKURU YAONYA UHUJUMU WA MIRADI

MKUU wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Pwani...

UKURASA WA 8

### WAJAWAZITO WALIA KUKOSA KITUO CHA AFYA

WAJAWAZITO Kijiji cha Kamara, Kata ya Mgonya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, wanalazimika kutumia zaidi ya Sh. 50,000 kukodi gari kufuatа huduma katika Kituo...

## Shahidi adai hatambui kama kina Mbowe walipanga kufanya ugaidi

UKURASA 2

MICHEZO KIIZA: NILIWAZIDI AKILI MABEKI WA SIMBA SC UK.24
MAONI, KATUNI UK.6

# Shahidi adai hatambui kama kina Mbowe walipanga ugaidi

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa 12 wa Jamhuri katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu, Luteni Dennis Urio, amedai kuwa hatambui kama washtakiwa hao walipanga vitendo vya kigaidi.

Sambamba na madai hayo, Urio amedai kuwa anafahamu baada ya kesi hiyo kumalizika, anaweza kuwa shujaa au mtu asiye na thamani duniani.

Akihojiwa jana na Wakili wa Utetezi, Nashon Nkungu, katika Mahakama Kuu, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mbele ya Jaji Joachim Tiganga, Luteni Urio alidai hafahamu kama Mbowe, Halfani Bwire, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya walikutana Morogoro, Moshi na Arusha kula njama za kufanya ugaidi.

Shahidi huo pia alikiri kwamba Mbowe hajawahi kukutana na makomandoo hao Morogoro bali yeye ndiye alikutana nao. Pia alikana kwamba alikwenda Morogoro kukutana na magaidi kuwaunganisha ili wafanye ugaidi.

Shahidi huyo alidai kuwa aliwadanganya mshtakiwa wa pili, Kasekwa, na wa tatu, Ling'wenya, kwamba kuna kazi ya ulinzi kwa Mbowe wakati anajua alitaka vijana hao kwa ajili ya kuambatana nao. Pia alikiri kumdanganya Mbowe wakati anamdodosa kuhusu ngazi yake ya kijeshi na kuwa hana ngazi yoyote.

Alidai kuwa katika mazungumzo yake na Mbowe, hapakuwa na umuhimu wa kutumia simu kurekodi kila anapopigiwa na Mbowe.

Wakili Nkungu alimtaka shahidi aonyeshe ujumbe mfupi wa simu inayozungumzia ugaidi katika simu yake iliyoko mahakamani kama kielelezo ndipo alipodai kuwa hakuna ujumbe unaozungumzia jambo hilo.

Urio alidai kuwa ujumbe uliomo ni wa kuwasafirisha vijana lakini hakuna neno ugaidi. Alidai kuwa ujumbe mmojawapo unasema: "Kaka wale mtu tatu wana uharaka siku zimeisha."

Kadhalika, shahidi huyo alidai kuwa moja ya ujumbe wa maandishi alimwambia Mbowe simu si salama kwa sababu walikuwa hawaelewani.

Awali, Luteni Urio aliibua mvutano wa kisheria baada ya kukataa kujibu baadhi ya maswali aliyokuwa akiulizwa na Wakili Nkungu akidai ni siri.

Wakili Nkungu akihoji maswali, alitaka kufahamu kama shahidi anajua baada ya kesi hiyo ya ugaidi ya Mbowe kumalizika anaweza kutoka shujaa au mtu asiye na thamani duaniani.

Luteni Urio alijibu kwamba anafahamu hilo na anaufahamu pia msemo usemao heri kufa jasiri kuliko kuishi kama mtumwa. Shahidi pia alikiri kwamba anajua kesi hiyo inafuatiliwa duniani kote.

Alipohojiwa kwa mwaka wanatoa makomandoo wangapi, pia alidai hawezi kusema ndipo alipobanwa zaidi na kuulizwa kama ana kiburi kutokana na kujibu maswali kisha akajibu kwamba amekula kiapo, hivyo hawezi kutoa siri.

Baada ya hapo, Nkungu alisimama na kudai: "Mheshimiwa Jaji kifungu 264 kinasema Mahakama Kuu itakuwa na mamlaka kuwa shahidi anapofika aweze kutoa ushahidi na shahidi amefika hataki kutoa majibu. Tunaomba mahakama itoe mwongozo."

"Tunaomba kiapo alichokula mahakamani kiwe juu ya viapo vingine vyote. Hakuna sheria inayokataza, kiusalama hakuna mambo ambayo yanakiukwa. Hatuoni shida kusema yeye ni nani. Wamekuja watu hapa wakasema wao ma-inspekta, ma- RCO."

"Kuna msemo unasema mwosha huoshwa. Katika mahakama hii, Wakili Abdallah Chavula ndiye alisimama kuhoji mashahidi kina Adamoo kwamba komandoo mmoja anapiga askari wangapi? Hatukipinga tulimuacha aulize.

"Tunaomba haki iwe pande mbili. Vifungu 141, 156,155 na 158 ni vifungu wezeshi ambavyo vinaipa mahakama wajibu wa kutoa ushahidi," alidai Nashon kasha Wakili Chavula akasimama na kuomba hoja za utetezi zisikubaliwe kwa kuwa hazina mashiko kisheria na kwamba shahidi hawezi kulazimishwa ajibu maswali.

Alidai Wakili anaomba mahakama imlazimishe shahidi kujibu swali lake, shahidi kasema siri hawezi kutamka hadharani ana nafasi gani.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar, pia aliungana na Chavula kuiomba mahakama itupilie mbali maombi ya utetezi na kwamba wakili aelekezwe kuuliza maswali sahihi.

Baada ya kusikiliza malumbano hayo, Jaji Tiganga aliahirisha hadi saa 8:30 mchana ili kuzipitia hoja hizo kisha kutoa uamuzi kama shahidi ajibu maswali hayo au asijibu.

Hata hivyo, Jaji alitoa uamuzi kwamba shahidi ajibu maswali na kwamba endapo mengine yatakuwa nje ya mipaka, ataelekeza asijibu.

Akitoa uamuzi, Jaji Tiganga alisema anakubaliana na Wakili Nkungu kwamba Kifungu cha 264 kinatoa mamlaka ya jumla juu ya Mahakama kuendesha shughuli zake.




Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Kati wa Benki ya CRDB, Boma Raballa (wapili kushoto), akikabidhi mfano wa tiketi ya kushuhudia mechi ya fainali ya Mashindano ya AFCON nchini Cameroon mmoja wa washindi wa droo ya Shinda na TemboCard Viza, Njama Ayoub Matumbo (kulia), wakati wa hafla ya kuwazawadia washindi wa mwezi Desemba 2021, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais Samia ataja matukio matano katika maisha yake

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametaja mambo matano aliyokutana nayo kwenye maisha na uongozi ikiwamo anavyokabiliana na wingi wa mafaili ofisini.

Samia aliyasema hayo jana Ikulu, Chamwino jijini hapo wakati akihojiwa katika kipindi cha Jambo Tanzania, kinachorushwa na kituo cha runinga cha TBC ikiwa ni kusherehekea siku yake ya kuzaliwa. Samia jana alitimiza umri wa miaka 62.

Alisema mafaili yanayowasilishwa ofisini kwake ni mengi na anajitahidi kuyafanyia kazi na kujikuta akilala saa saba ya usiku.

"Mafaili yapo hadi kitandani najitahidi yasikae kwangu, yakakae huko kwa wenzangu. Kila yakiingia mimi nayatoa na muda mwingi najikuta kulala ni saa 7:00 za usiku.

"Nikilala na faili juu ya meza siku hiyo nimechoka sana, lakini mara nyingi najitahidi nisilale na faili juu ya meza. Lakini ukiacha mafaili kazi ni nyingi pia wanaotaka uende ukarasmishe shughuli zao, wanaotaka ukawatembelee, unaalikwa nje, unaowaalika waje, kazi ni nyingi sana," alisema.

"Ukijua kuwatumia wasaidizi huwi na mzigo mkubwa kwa sababu unaurudisha kwa wasaidizi na wao wafanye ndiyo maana katika mikutano mingi na wasaidizi wangu nawaambia amueni fanyeni maamuzi (uamuzi)," aliongeza.

Kuhusu wanaokosea kufanya uamuzi, atamrekebisha hata mara nne na kwamba hatamfukuza isipokuwa amerudia mara nyingi kufanya hivyo.

Mbali na kukumbana na mzigo wa mafaili, Rais Samia alitaja jambo lingine alilokutana nalo ni kero za Muungano. Alisema alipokuwa Waziri katika Serikali ya Zanzibar, alikuwa msemaji na alipoteuliwa kuwa Waziri wa Muungano, alipewa jukumu hilo na kupunguza kero 12 kutoka zaidi ya 20 zilizokuwapo.

### BUNGE LA KATIBA

Mwaka 2014 katika Bunge la Katiba, alikuwa makamu mwenyekiti huku mwenyekiti akiwa Samuel Sitta (sasa marehemu). Alisema katika kipindi hicho ufanisi mkubwa ulitokana na namna walivyopata theluthi mbili ya wajumbe kutoka Zanzibar kupitisha rasimu ya Katiba Inayopendekezwa.

"Namshukuru Mungu kwenye Bunge tulitoka vyema. Kikwazo kikubwa kilikuwa kupata theluthi mbili kutoka Zanzibar kusema ndiyo kwa ile rasimu ya Katiba tuliyokuja nayo. Ilikuwa kazi sana kwa sababu kule sisi tulikuwa tumegawanyika nusu hawa nusu. Ilikuwa kazi kuzungumza na ndugu zangu, kuwaelewesha, kuwashawishi mpaka tukafanikiwa kuipata hiyo idadi," alisema.

### MGOMBEA MWENZA

Kiongozi huyo alisema tukio ambalo lilimstaajabisha mwaka 2015 ni wana CCM kumpitisha kuwa mgombea mwenza wa mgombea urais ambaye alikuwa Dk. John Magufuli (marehemu).

"Lakini nikasema Mungu akipanga anakupa njia. Kwa hiyo tukaenda nalo tukavuka salama," alisema.

### KIFO CHA MAGUFULI

Kifo cha Magufuli, alisema kilikuwa kubwa kushinda yote kutokana na kuondokewa na kiongozi mkuu wa nchi, hivyo yeye kulazimika kushika usukani wa kuongoza nchi. "Ilikuwa 'shock' (mshtuko) ya maisha yangu, lakini Mungu akipanga, Mungu anakupa njia."

Anakupa maono na kukuelekeza cha kufanya ilmradi kuwa na nia ya dhati kulifanya lile ambalo wenzako wametaka mlifanye basi tunakwenda," alisema.

### KUPERUZI MITANDAONI

Rais Samia alisema anapopata nafasi ya kupumzika, hutumia kuongeza ujuzi wa kazi kwa kuangalia wanavyofanya wengine. "Nikiingia kwenye mitandao naona mambo haya yametokea wapi yalipotokea yamechukuliwa hatua gani, labda wapi kuna nini kuna changamoto zipi zinafanana na nchi gani. Unaingia kuangalia walivyofanya nyuma au sasa hivi jinsi ya kushughulika na changamoto zinazokuja," alisema.

### UJUMBE KWA WATANZANIA

"Huwa nawaambia duniani kuna nchi moja tu inayoitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakuna nyingine. Ndani yake kuna Watanzania ambao ni sisi na Mungu ametupanga katika ngazi mbalimbali. Wito wangu tufanye kazi kwa bidii. Tutakaojenga nchi hii ni sisi Watanzania na tutakaobomoa ni sisi Watanzania," alisema.

Aliwataka Watanzania kufuata mila, desturi, Katiba, sheria za nchi na taratibu zilizowekwa na kujituma kufanya kazi kwa bidii kwa kila ngazi ili kuiinua zaidi nchi.

## HABARI KITAIFA

# Mzee wa miaka 80 ajinyonga hadi kufa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma limethibitisha kutokea kwa tukio la mzee mwenye umri wa miaka 80, Edward Lusito, anayedaiwa kujinyonga hadi kufa katika eneo la Njedengwa, mkoani hapo.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa mzee huyo alikutwa amejinyonga kwa kutumia kamba ya katani chumbani kwake hadi kufa usiku wa kuamkia jana.

Akizungumza na Nipashe, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga, alisema tukio hilo lilitokea jana na jeshi hilo limeanza uchunguzi ili kubaini sababu za kujinyonga kwake.

Tukio hilo ni la nne katika kipindi cha wiki mbili, likiwamo la wanawake wawili kuuawa kikatili na wenza wao, mauaji ya familia ya watu watano na watoto wa mitaani kuchomana na visu na kusababisha kifo cha mtoto mmoja.

Kamanda Lyanga alisema mzee huyo alijinyonga mwenyewe na polisi inaendelea na uchunguzi kwa ajili ya kubaini chanzo cha matukio ya kujitoa na kutoana uhai.

Alisema Jeshi la Polisi halitavumilia vitendo vya kihalifu vinavyofanywa na jamii kwa sababu havikubaliki na wataendelea kukemea ili kuhakikisha jamii inaacha kufanya matukio hayo.

Vile vile, alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi wa matukio yote ya mauaji na uhalifu yanayofanywa na jamii na kuwachukulia hatua za kisheria wanaohusika.

Aliwataka wananchi wa Dodoma kuendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo ili kuwabaini wahalifu wanaofanya vitendo hivyo kwa jamii na kukatiza maisha yao.

Juzi Makamu wa Rais Philip Mpango kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, alikemea vitendo hivyo na kutaka polisi kuchukua hatua kukomesha matukio hayo ya mauaji.

# TAKUKURU yaonya uhujumu wa miradi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Pwani, Suzana Raymond, amewaonya watu wenye nia ya kuihujumu serikali kwenye miradi ya maendeleo kuwa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Suzana alitoa kauli hiyo jana mjini Kibaha alipokuwa akitoa taarifa ya miezi mitatu ya taasisi hiyo kwa waandishi wa habari.

"Tutakuwa wakali sana kwa watu wanaojihusisha na rushwa au ufisadi kwenye miradi ya maendeleo, tuungane pamoja kujenga Tanzania yenye maendeleo ya kweli kupitia miradi hiyo inayoanzishwa na serikali yetu," alisema Suzana.

Aliwaomba wakazi wa Mkoa wa Pwani kufuatilia miradi ya maendeleo katika maeneo yao na kutoa taarifa wanapokuwa na shaka kuhusiana na utekelezaji wa miradi hiyo. "Katika usimamizi wa miradi tutangulize uzalendo tuwe waaminifu na waadilifu ili kujenga Tanzania imara kadri ya maelekezo ya serikali," alisisitiza.

Alieleza kuwa katika kipindi cha miezi mitatu miradi ya maendeleo 56 katika sekta za afya, elimu na maji yenye thamani ya Sh. bilioni 11.9 ilikaguliwa.

Alisema katika ukaguzi mapungufu yaliyobainika yalifanyiwa marekebisho ili kuhakikisha miradi inalingana na thamani ya fedha.

Katika kipindi hicho pia malalamiko 132 yalipokelewa katika taasisi hiyo ambapo kati ya hayo 93 yalihusu rushwa, na kwamba 92 uchunguzi wake unaendelea na moja uchunguzi umekamilika.

# Polisi Dar yaua watatu kwa tuhuma ujambazi

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam limesema limewaua watu watatu wanaodaiwa kuwa ni majambazi katika eneo la Mbagala Zakhem mkoani Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi Kanda hiyo, Jumanne Muliro, alimtaja mmoja wa watu hao ni Mrisho Bonge ambaye alikuwa na wenzake wawili, ambao walikuwa katika harakati za kwenda kufanya tukio la uporaji katika duka linalotoa huduma za kifedha.

Kamanda Muliro alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya usiku karibu na duka la Rosemary Kimario ambaye ni wakala wa huduma za kifedha.

Alisema watuhumiwa hao wakiwa na pikipiki yenye namba MC 908 DBG walifika katika eneo hilo na wakiwa katika hatua za mwisho za kutaka kuvamia na kupora pesa walibaini kuwa wanafuatiliwa na askari polisi ambao walifika haraka katika eneo hilo.

"Watu hao baada ya kubaini kuwa wanafuatiliwa walianza kurusha risasi ovyo, askari polisi katika mazingira hayo walijihami na kuwashambulia watuhumiwa hao ambao walijeruhiwa na kupelekwa haraka hospitali, lakini baada ya kufikishwa ilibainika wamepoteza maisha," alisema Muliro.

Kamanda Muliro alisema katika eneo la tukio watuhumiwa hao walikutwa na bastola moja aina ya model 75 CAL 9 Para namba K4596 ikiwa na magazine moja yenye risasi 11.

Alisema watu hao pia walikutwa na noti bandia zenye thamani ya Sh.milioni moja, ambazo huzitumia kuwazubaisha mawakala kama wateja na baadaye huwapora fedha halisi kwa kuwatishia na silaha.

Kamanda Muliro alisema: "Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawataka raia wema kuendelea kutoa taarifa za kihalifu mapema ili Jeshi la Polisi kufanya kazi ya kuzuia matukio hayo."


## Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationship beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

## PUBLICATION OF FINANCIAL STATEMENTS

**Issued pursuant to regulations 7 and 8 of the Banking and Financial Institutions (Disclosures) Regulations, 2014**

### CONDENSED STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31 DECEMBER 2021
(Amounts in million shillings)

| | | Current Quarter 31-Dec-21 | Previous Quarter 30-Sep-21 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **ASSETS** | | |
| 1 | Cash | 1,905 | 1,521 |
| 2 | Balances with Bank of Tanzania | 16,405 | 12,176 |
| 3 | Investments in Government securities | 51,033 | 52,660 |
| 4 | Balances with other banks and financial institutions | 1,663 | 2,238 |
| 5 | Cheques and items for clearing | - | - |
| 6 | Inter branch float items | - | - |
| 7 | Bills negotiated | - | - |
| 8 | Customers' liabilities for acceptances | - | - |
| 9 | Interbank Loans Receivables | 23,972 | 19,370 |
| 10 | Investments in other securities | - | - |
| 11 | Loans, advances and overdrafts (net of allowances for probable losses) | 70,516 | 74,893 |
| 12 | Other assets | 2,678 | 2,845 |
| 13 | Equity Investments | - | - |
| 14 | Underwriting accounts | - | - |
| 15 | Property, Plant and Equipment | 1,383 | 1,540 |
| **16** | **TOTAL ASSETS** | **169,555** | **167,243** |
| **B.** | **LIABILITIES** | | |
| 17 | Deposits from other banks and financial institutions | 57,932 | 56,071 |
| 18 | Customer deposits | 70,561 | 70,437 |
| 19 | Cash letters of credit | - | - |
| 20 | Special deposits | - | - |
| 21 | Payment orders/transfers payable | 28 | 31 |
| 22 | Bankers' cheques and drafts issued | 25 | 25 |
| 23 | Accrued taxes and expenses payable | 2,611 | 2,415 |
| 24 | Acceptances outstanding | - | - |
| 25 | Interbranch float items | - | - |
| 26 | Unearned income and other deferred charges | - | - |
| 27 | Other liabilities | 701 | 1,107 |
| 28 | Borrowings | - | - |
| **29** | **TOTAL LIABILITIES** | **131,858** | **130,086** |
| **30** | **NET ASSETS/(LIABILITIES)*(16 minus 29)*** | **37,697** | **37,157** |
| **C.** | **SHAREHOLDERS' FUNDS** | | |
| 31 | Paid up share capital | 21,500 | 21,500 |
| 32 | Capital reserves | 1,911 | 2,222 |
| 33 | Retained earnings | 12,580 | 12,269 |
| 34 | Profit (Loss) account | 1,706 | 1,166 |
| 35 | Other capital accounts | - | - |
| 36 | Minority Interest | - | - |
| | | - | - |
| **37** | **TOTAL SHAREHOLDERS' FUNDS** | **37,697** | **37,157** |
| 38 | Contingent liabilities | 9,516 | 7,523 |
| 39 | Non performing loans & advances | 2,081 | 2,129 |
| 40 | Allowances for probable losses | 636 | 455 |
| 41 | Other non performing assets | - | - |
| **D.** | **SELECTED FINANCIAL CONDITION INDICATORS** | | |
| (i) | Shareholders Funds to total assets | 22.23% | 22.22% |
| (ii) | Non performing loans to total gross loans | 2.92% | 2.82% |
| (iii) | Gross loans and advances to total deposits | 55.37% | 59.56% |
| (iv) | Loans and Advances to total assets | 41.59% | 44.78% |
| (v) | Earning Assets to Total Assets | 86.20% | 88.12% |
| (vi) | Deposits Growth | 1.57% | 3.09% |
| (vii) | Assets growth | 1.38% | 2.85% |

### CONDENSED STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME FOR THE QUARTER ENDED 31 DECEMBER 2021
(Amounts in million shillings)

| | | Current Quarter | Comparative Quarter (Previous Year) | Current Year Cumulative | Comparative Year (Previous Year) Cumulative |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31-Dec-21 | 31-Dec-20 | 31-Dec-21 | 31-Dec-20 |
| 1 | Interest Income | 3,274 | 3,191 | 12,691 | 12,490 |
| 2 | Interest Expense | 1,173 | 1,295 | 4,713 | 5,014 |
| **3** | **Net Interest Income (1 minus 2)** | **2,101** | **1,896** | **7,978** | **7,476** |
| 4 | Bad Debts Written-Off | (201) | 175 | (198) | 182 |
| 5 | Impairment Losses on Loans and Advances | 472 | (274) | 1,163 | 656 |
| **6** | **Non Interest Income:** | **426** | **189** | **927** | **697** |
| | 6.1 Foreign Currency Dealings and Translation Gains/(Loss) | 50 | 34 | 166 | 188 |
| | 6.2 Fees and Commissions | 376 | 155 | 761 | 509 |
| | 6.3 Dividend Income | - | - | - | - |
| | 6.4 Other Operating Income | - | - | - | - |
| **7** | **Non Interest Expenses:** | **1,497** | **1,326** | **5,358** | **4,699** |
| | 7.1 Salaries and Benefits | 585 | 457 | 2,155 | 1,743 |
| | 7.2 Fees and Commission | - | - | - | - |
| | 7.3 Other Operating Expenses | 912 | 869 | 3,203 | 2,956 |
| **8** | **Operating Income/(Loss)** | **759** | **858** | **2,582** | **2,636** |
| 9 | Income Tax Provision | 219 | - | 876 | 537 |
| **10** | **Net Income/ (Loss) After Income Tax** | **540** | **858** | **1,706** | **2,099** |
| 11 | **Other Comprehensive Income (itemize)** | - | - | - | - |
| **12** | **Total comprehensive income/(loss) for the quarter** | **540** | **858** | **1,706** | **2,099** |
| 13 | Number of Employees | 32 | 30 | 32 | 30 |
| 14 | Basic Earnings Per Share | 101 | 160 | 159 | 98 |
| 15 | **Number of Branches** | 2 | 2 | 2 | 2 |
| | **SELECTED PERFORMANCE INDICATORS** | | | | |
| (i) | Return on Average Total Assets | 1.81% | 2.11% | 1.57% | 1.68% |
| (ii) | Return on Average Shareholders' Fund | 5.73% | 9.35% | 4.61% | 5.81% |
| (iii) | Non Interest Expense to Gross Income | 40.46% | 39.23% | 39.34% | 35.63% |
| (iv) | Net Interest Income to Average Earning Assets | 5.78% | 5.39% | 5.68% | 5.58% |

### CONDENSED STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY AS AT 31 DECEMBER 2021
(Amounts in million shillings)

| | Share Capital | Share Premium | Retained Earnings | Regulatory Reserve | General Reserve | Others | Total |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Current Quarter 2021** | | | | | | | |
| **Balance as at the beginning of the quarter 01.10.2021** | **21,500** | - | **13,435** | **2,222** | - | - | **37,157** |
| Profit for the the quarter | - | - | 540 | - | - | - | **540** |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | - | - |
| Transactions with owners | - | - | - | - | - | - | - |
| Dividends Proposed | - | - | - | - | - | - | - |
| Regulatory Reserve | - | - | 310 | (310) | - | - | - |
| General Provision Reserve | - | - | - | - | - | | - |
| Loan written off | - | - | - | - | - | - | - |
| Others | - | - | - | - | - | - | - |
| **Balance as at the end of the quarter 31.12.2021** | **21,500** | - | **14,286** | **1,911** | - | - | **37,697** |
| **Previous Quarter 2021** | | | | | | | |
| **Balance as at the beginning of the quarter 01.07.2021** | **21,500** | - | **12,424** | **2,222** | - | - | **36,146** |
| Profit for the quarter | - | - | 1,012 | - | - | - | **1,012** |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | - | - |
| Transactions with owners | - | - | - | - | - | - | - |
| Dividends Proposed | - | - | - | - | - | - | - |
| Regulatory Reserve | - | - | - | - | - | - | - |
| General Provision Reserve | - | - | - | - | - | - | - |
| Loan written off | - | - | - | - | - | - | - |
| Others | - | - | - | - | - | - | - |
| **Balance as at the end of the quarter 30.09.2021** | **21,500** | - | **13,435** | **2,222** | - | - | **37,157** |

### CONDENSED STATEMENT OF CASH FLOW STATEMENT FOR THE QUARTER ENDED 31 DECEMBER 2021
(Amounts in million shillings)

| | | Current Quarter | Previous Quarter | Current Year Cumulative | Comparative Year (Previous Year) Cumulative |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31-Dec-21 | 30-Sep-21 | 31-Dec-21 | 31-Dec-20 |
| **I:** | **Cash flow from operating activities:** | | | | |
| | Net income(loss) | 759 | 1,231 | 2,582 | 2,636 |
| | Adjustments for: | | | | - |
| | - Impairment/Amortization | 712 | 555 | 1,332 | 1,406 |
| | - Net change in Loans and Advances | 3,816 | (4,056) | 2,662 | (2,224) |
| | - Gain/loss on Sale of Assets | - | - | - | - |
| | - Net change in Deposits | 1,985 | 3,793 | 6,984 | 14,351 |
| | - Net change in Short Term Negotiable Securities | 4,409 | (3,809) | 66 | (839) |
| | - Net change in Other Liabilities | (212) | (174) | (591) | (602) |
| | - Net change in Other Assets | (3,214) | (758) | 666 | (4,131) |
| | - Tax Paid | (219) | (219) | (876) | (886) |
| | - Others (specify) | - | - | - | - |
| | ***Net cash provided (used) by operating activities*** | ***8,037*** | ***(3,437)*** | ***12,825*** | ***9,710*** |
| **II:** | **Cash flow from investing activities:** | | | | - |
| | Dividend Received | - | - | - | - |
| | Purchase of Fixed Assets | (63) | (40) | (273) | (215) |
| | Proceeds from Sale of Fixed Assets | - | - | - | - |
| | Purchase of Non- Dealing Securities | - | - | - | - |
| | Proceeds from Sale of Non-Dealing Securities | - | - | - | - |
| | Others (specify) | - | - | - | - |
| | ***Net cash provided (used) by investing activities*** | ***(63)*** | ***(40)*** | ***(273)*** | ***(215)*** |
| **III:** | **Cash flow from financing activities:** | | | | |
| | Repayment of Long-term Debt | - | - | - | - |
| | Proceeds from Issuance of Long Term Debt | - | - | - | - |
| | Proceeds from Issuance of Share Capital | - | - | - | - |
| | Payment of Cash Dividends | - | - | - | - |
| | Net Change in Other Borrowings | - | - | - | (387) |
| | Others (specify) | - | - | - | - |
| | ***Net Cash Provided (used) by Financing Activities*** | - | - | - | **(387)** |
| **IV:** | **Cash and Cash Equivalents:** | | | | |
| | **Net Increase/ (Decrease) in Cash and Cash Equivalents** | **7,974** | **(3,477)** | **12,552** | **9,108** |
| | Cash and Cash Equivalents at the Beginning of the Quarter | 37,118 | 40,595 | 32,540 | 23,432 |
| | **Cash and Cash Equivalents at the end of the Quarter** | **45,092** | **37,118** | **45,092** | **32,540** |

### SELECTED EXPLANATORY NOTES FOR THE QUARTER ENDED 31 DECEMBER 2021

In preparation of the quarterly financial statements, consistent accounting policies have been used as those applicable to the previous year audited financial statements

| Name and Title | Signature | Date |
|---|---|---|
| Mr. Antaryami Sarangi<br>Managing Director | | 20.01.2022 |
| Mr. Heriabdiel Ayoh<br>General Manager | | 20.01.2022 |
| Mr. Allen Richard<br>Internal Auditor | | 20.01.2022 |

We, the undersigned directors, attest to the faithful representation of the above statements. We declare that the statements have been examined by us and, to the best of our knowledge and belief, have been prepared in conformance with International Financial Reporting Standards and the requirements of the Banking and Financial Institutions Act, 2006 and they present a true and fair view.

| Name | Signature | Date |
|---|---|---|
| 1. Mr. Suitbert Kageuka - Director | | 20.01.2022 |
| 2. Dr. Paul Kato - Director | | 20.01.2022 |

# PM atoa maagizo 13 kuhusu Kiswahili

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa maagizo 13 kwa chuo kikuu, mabalozi, wizara, mahakama na taasisi kuhakikisha lugha ya Kiswahili inaimarishwa kwa kufundishwa na kutumika kimataifa ili kutengeneza jina duniani kuwa chimbuko lake lilianzia hapa.

Majaliwa alitoa maagizo hayo jana wakati wa utoaji wa tuzo za Kiswahili ya mabati-Cornell ya Fasihi ya Afrika za mwaka 2021 zilizoandaliwa na kudhaminiwa na Kampuni ya mabati ya ALAF kwa kushirikiana na Kampuni ya mabati ya Rolling Mills ya Kenya ambazo ni miongoni mwa kampuni za Safal Mauritius.

Ofisi nyingine iliyoshiriki ni ya Makamu Mkuu wa Masuala ya kimataifa katika Chuo Kikuu cha Cornell, Idara ya Taaluma za Afrika ya Chuo Kikuu cha Cornell, Marekani.

Majaliwa aliagiza matumizi fasaha ya Kiswahili yapewe kipaumbele kwenye huduma za jamii, mikutano, mahakamani, warsha na makongamano yote ya ndani na nje.

"Pili, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, iendelee kuufanyia kazi mkakati wa kukitumia Kiswahili kufundisha katika ngazi mbalimbali za elimu na kuongeza wataalamu wa Kiswahili.

"Wizara ya Elimu, Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo na Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki shirikianeni kujenga uwezo wa wataalamu wa ndani wa kutafsiri lugha mbalimbali za kigeni."

Jambo la tatu, amezitaka balozi zote za nje zianzishe madarasa ya Kiswahili kwenye nchi wanazoziwakilisha ili wanaotaka wajifunze huko na kutolea mfano balozi wa Zambia, Cuba, Canada, Ufaransa tayari wameshafanya hivyo.

Nne, Majaliwa amewataka wataalamu wa Kiswahili wahakikishe wanaweka mikakati thabiti ili kukipenyeza kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandika kamusi na vitabu vitakavyosaidia watu kujifunza lugha hiyo.

Ametaka baadhi ya maeneo watumie mbinu za ushawishi ili kukifikisha kwenye maeneo yao hususan katika medali za kimataifa.

Tano ametaka mafunzo ya Kiswahili yaimarishwe kwa kutoa programu maalumu za kuzalisha wataalamu na wakalimani wa lugha hii wenye kukidhi viwango vya kimataifa.

Jambo la sita alilitoa kwa taasisi za elimu kuanzisha utaratibu wa kuwatambua wataalamu katika ngazi za umahiri ili washindane katika soko la ajira kwa sababu wakati fulani watanzania walishindwa kufanya hivyo kutokana na kutokuwa na vyeti vya kutambua umahiri wao katika Kiswahili.

"Saba, matumizi yake yaimarishwe katika kutoa huduma za kimahakama na uandishi wa nyaraka za kisheria ambayo pia najua yanaendelea pamoja na kutafsiri sheria. Nane, mikakati madhubuti iwekwe ili kuridhiwa kuwa lugha rasmi kwenye jumuiya nyingine za kikanda na kimataifa."




Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa NSSF, Balozi Ali Idi Siwa (kushoto), akikabidhi zawadi ya picha kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alipofanya ziara ya kikazi katika ofisi ya NSSF makao makuu, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndalichako aipongeza NSSF kufikia wanachama sekta rasmi, isiyo rasmi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Profesa Joyce Ndalichako, amepongeza kazi inayofanywa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa kuifikia sekta rasmi na sekta isiyo rasmi.

Pia, amefurahishwa na uongozi wa Mfuko ulivyofanikiwa kuongeza idadi ya wanachama na kufanya thamani yake kuendelea kukua.

Profesa Ndalichako alisema hayo jana katika ziara yake makao makuu ya NSSF jijini Dar es Salaam, ikiwa ni mara yake ya kwanza tangu alipoteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kushika wadhifa huo.

Aliupongeza Mfuko kwa kupata mafanikio mbalimbali na kuwaomba kuongeza juhudi za kufuatilia michango ya wanachama kutokana na baadhi ya waajiri wa sekta binafsi kuwa na changamoto ya kutowasilisha michango ya wanachama wao kwa wakati.

Alisema kazi nzuri inayoendelea kufanywa na watumishi wa Mfuko inaleta matokeo chanya hasa katika kuongeza idadi ya wanachama kutoka sekta binafsi na isiyo rasmi jambo linalosaidia makusanyo kuzidi kuongezeka.

Profesa Ndalichako alikiri kuwa ndani ya mwaka mmoja malalamiko ya wanachama wa NSSF yamepungua tofauti na ilivyokuwa kipindi cha nyuma kwa baadhi ya wanachama kuomba msaada ili waweze kulipwa mafao yao.

"Ukweli ni kwamba sasa malalamiko mengi yamepungua na taarifa niliyopatiwa hali inakwenda vizuri...nawapongeza sana kwa kazi nzuri mnayofanya ya kuwahudumia Watanzania na kuwapa elimu ya kujiwekea akiba kwa ajili ya maisha yao ya sasa na ya baadaye," alisema.

Hata hivyo, aliuomba uongozi wa NSSF kuweka mkazo katika sekta isiyo rasmi kwa sababu inakua kwa kasi na waendelee kutoa elimu kwa wajasiriamali mbalimbali wakiwamo mama lishe, bodoboda, wavuvi, wakulima, wachimbaji wadogo wa madini pamoja na wajasiriamali wengine wote waweze kujiunga kwa ajili ya kujiwekea akiba ya uzeeni.

Profesa Ndalichako alifurahishwa na Mfuko ulivyojipanga kufikisha huduma zake kwa kutumia mifumo mbalimbali ya TEHAMA hatua inayorahisisha zaidi upatikanaji wa huduma na kuwafikia wanachama wengi.

Profesa Ndalichakao aliupongeza Mfuko kwa kufanya uwekezaji ambao ni moja ya jukumu lao la msingi na kwamba ameona miradi mingi wanayofanya ya uwekezaji na kuwaasa yenye changamoto waendelee kuchukua hatua ili kuikwamua.

Awali, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Partobas Katambi, alisema mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Mfuko huo yanatokana na kazi kubwa inayofanywa na watumishi wa NSSF hasa katika kutekeleza majukumu ya msingi.

# LHRC sasa yalaani matukio ya mauaji

**Na Christina Mwakangale**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimelaani matukio ya mauaji yanayoendelea kutokea maeneo mbalimbali nchini, hususani yaliyoripotiwa Januari, mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana, alisema katika kipindi cha Januari mwaka huu takribani matukio 20 yameripotiwa na kusababisha ukiukwaji wa haki za binadamu.

Kutokana na matukio hayo kukithiri, alisema LHRC inatoa wito kwa wanasaikolojia, watetezi wa haki za binadamu pamoja na viongozi wa kijamii kutumia muda wao kuuelimisha umma.

"Kituo cha sheria kimekusanya takribani matukio 20 ya mauaji hayo, yaliyoripotiwa katika mikoa ya Mtwara, Rukwa, Njombe, Katavi, Mwanza, Dodoma, Ruvuma, Dar es Salaam na Mara,"alisema Henga.

Alisema tukio lingine lililotokea mkoani Mwanza, liliripotiwa wanawake watatu kuuawa na miili yao kutupwa eneo la Mecco Kusini, wilayani Ilemela Januari 20 mwaka huu. "Ilidaiwa kwamba wanawake hao walibakwa kisha kuuawa kikatili kwa kukatwa na mapanga na watu wasiojulikana. LHRC inalaani kitendo hiki cha ukatili dhidi ya wanawake na tunatoa rai kwa Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi na kuhakikisha watu waliofanya vitendo hivi vya ukatili wanafikishwa mahakamani," alisema Henga.

Kadhalika, alisema tukio lingine ni lililotokea mkoani Rukwa, kulikoripotiwa mauaji ya mama na watoto wake wawili, mmoja wa umri wa miaka mitatu na mwingine sita, waliouawa katika mazingira ya kutatanisha na watu wasiojulikana na miili yao kukutwa imekatwa sehemu mbalimbali.

Alisema tukio lingine lilitokea mkoani Dodoma, Januari 23, mwaka huu, kuliko ripotiwa tukio la watu watano wa familia moja, kuuawa na watu wasiojulikana katika Kijiji cha Zanka wilayani Bahi.

"LHRC imerekodi tukio la mauaji wilayani Songea mkoani Ruvuma, kwamba mhudumu wa nyumba ya kulala wageni ya Peace Lodge, Gema Haule (23), aliuawa kikatili na mteja katika nyumba hiyo ya kulala wageni.

"Mteja huyo alikuwa anadaiwa Sh. 50,000. Kutokana na deni hilo, uongozi wa nyumba hiyo ya kulala wageni, uliamua kushikilia simu ya mkononi ya mteja huyo aina ya Nokia na nguo zake hadi pale atakapolipa deni hilo," alieleza Anna na kuongeza:

Hata hivyo, mteja huyo aligoma kulipa deni na kuendelea kuja mara kwa mara kudai vitu vyake. Januari 20 mteja huyo alifika tena kudai vitu hivyo na alipokataliwa ndipo akaamua kutekeleza mauaji hayo.

Yetu Microfinance Bank PLC
"Creating Wealth Together, Pamoja Tunaweza"

# YETU MICROFINANCE BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DECEMBER 2021.

| | | Robo Mwaka wa sasa 31-Dec-21 TZS | Robo Mwaka wa sasa 30-Sep-21 TZS |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 811,284,530 | 819,368,398 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 99,362,319 | 32,832,347 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | | |
| 4 | Salio katika Benki Nyinginezo na Taasisi za Fedha | 27,602,387 | 126,767,311 |
| 5 | Hundi na Miamala ya kushughulikiwa | | |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | | |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | | |
| 8 | Dhima za Wateja zilizokubalika | | |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | | |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | | |
| 11 | Mikopo Halisi iliyopo | 13,801,091,769 | 14,544,415,369 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,458,387,098 | 1,535,111,154 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | | |
| 14 | Akaunti za udhamini | | |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,773,501,419 | **1,711,129,297** |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | 17971229522 | **18,769,623,874** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | | |
| 18 | Amana za Wateja | 2,274,439,496 | 2,154,646,532 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | | |
| 20 | Amana Maalumu | 1,418,704,594 | 2,064,363,594 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | | |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | | |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | | |
| 24 | Dhima la Tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya Benki na Mteja | | |
| 25 | Miamala isiyoshughulikiwa baina ya Matawi | | |
| 26 | Mapato yalioingia ya kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa baadae | | |
| 27 | Dhima Nyingine | 277,852,173 | 229,836,593 |
| 28 | Madeni | 5,650,000,000 | 5,700,000,000 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **9,620,996,263** | **10,148,846,719** |
| 30 | **MALI/{DHIMA} HALISI** | **8,350,233,259** | **8,620,777,155** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 6,056,496,547 | 6,056,496,547 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | | |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | | |
| 34 | Faida/{Hasara} ya Kipindi Husika | 2,439,473,000 | 2,439,473,000 |
| 35 | Akaunti zingine za Mtaji | (207,854,619) | 56,434,051 |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa chache | 62,118,331 | 68,373,556 |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **8,350,233,259** | **8,620,777,155** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | **0** | |
| 39 | Mikopo chechefu | 3,194,085,725 | 4,448,185,825 |
| 40 | Tengo Kwa ajili ya mikopo chechefu | 605,675,243 | 717,420,694 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | % | % |
| i | Uwiano wa Fedha za wanahisa na Jumla ya Mali | 46.46% | 45.93% |
| ii | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo | 23.14% | 30.58% |
| iii | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 390% | 362% |
| iv | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 77% | 77% |
| v | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 80% | 81% |
| vi | Ongezeko la Amana | 1% | 1% |
| vii | Ongezeko la Mali | -2% | -1.72% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DECEMBER 2021.

| | | Robo Mwaka wa sasa 31-Dec-21 TZS | Robo Mwaka wa sasa 30-Sep-21 TZS | Limbikizo Robo Mwaka wa sasa 31-Dec-21 TZS |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 1,072,410,349 | 1,033,423,856 | 4,464,549,211 |
| 2 | Gharama za Riba | 109,311,397 | 150,931,913 | 458,922,410 |
| 3 | **Mapato Halisi (1 kutoa 2)** | **963,098,953** | **882,491,943** | 4,005,626,801 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | | 0.00 | 0 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika mikopo | -27,793,822 | -206,094,716 | -60,287,854 |
| 6 | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **151,597,635** | **163,690,836** | 854,483,042 |
| | | | 0 | 0 |
| | 6.1 Faida/(Hasara) zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | | | |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 110,717,422 | 103,803,732 | 441,670,915 |
| | 6.3 Gawio | | 0.00 | |
| | 6.4 Mapato Mengine | 40,880,213 | 59,887,105 | 412,812,127 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,439,425,580** | **1,171,657,422** | 4,838,847,257 |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 636,722,799 | 618,195,313 | 2,515,816,021 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 36,436,487 | 13035651.75 | 50,044,365 |
| | 7.3 Gharama nyingine | 766,266,294 | 540,426,457 | 2,272,986,871 |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **(296,935,170)** | **80,620,073** | 81,550,440 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (89,080,551) | 24,186,022 | 24,465,132 |
| 10 | **Faida/(Hasara ) Halisi baada ya Kodi ya Mapato** | **(207,854,619)** | **56,434,051** | 57,085,308 |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa{bainisha} | | **0.00** | |
| 12 | **Jumla ya Faida/{Hasara} iliyojumuishwa kwa Mwaka** | **(207,854,619)** | **56,434,051** | **57,085,308** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 129 | 129 | 129 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 13 | 13 | 13 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 3 | 3 | 3 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -1% | 5.50% | 0.45% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -2% | 12.00% | 1% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 71% | 52.00% | 51% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 7% | 6.00% | 29% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DECEMBER 2021

| | | Robo Mwaka wa sasa 31-Dec-21 TZS | Robo Mwaka wa sasa 30-Sep-21 TZS |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **(207,854,619)** | **56,434,051** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - |
| | - Faida/{Hasara} kwenye Mauzo ya Mali | | |
| | -Uchakavu wa Mali za Kudumu | **101,590,391** | **100,702,752** |
| | -Uchakavu wa Matengenezo Makubwa | - | - |
| | -Utumikaji wa Mtaji wa Misaada | | |
| | -Uchakavu wa Mali Zisizoshikika | - | - |
| | | **(106,264,229)** | **157,136,803** |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Salio la Benki Kuu ya Tanzania | | |
| | - Badiliko Halisi katika Mikopo | 743323599.9 | |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (76,724,056) | 134,287,250 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 119,792,964 | 797,660,627 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika salio la benki Nyingine na Taasisi za Fedha | (645,659,000) | 14,961,519 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 48,015,580 | 47,415,352 |
| | | **82,484,859** | **1,151,461,552** |
| | - Kodi Iliyolipwa | (89,080,551) | (32,000,000) |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(6,595,692)** | **1,119,461,552** |
| | | - | - |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | 62,372,122 | (40,555,242) |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Mali Zisizoshikika | - | - |
| | Mengineyo Amana za kudumu | - | - |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa*** | **62,372,122** | **(40,555,242)** |
| | | - | **0%** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | (50,000,000) | (955,619,586) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | | |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (46,495,249) | (47,415,352) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | | |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha* | **(96,495,249)** | **(1,003,034,938)** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko/ Punguzo Halisi katika Fedha taslimu na Mali zinazofanana | **(40,718,818)** | **75,871,372** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo | **978,968,055** | **903,096,683** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo | **938,249,237** | **978,968,055** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DECEMBER 2021 Kiwango kwa Tzs

| Kiwango kwa Tzs.'(000)' | Mtaji wa His | Mtaji mkuu wa kisheria | Mtaji wa kisheria | | Akaunti zingine za Mtaji | Tengo la ziada ya juma | Jumla Tzs |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Salio la wa mwaka 01/01/2020 | 6,056,497 | - | - | - | 69,693 | 2,332,349 | 8,458,539 |
| Rekebisho : | | | | | | - | - |
| Ongeza: Jumlisha/(Futa) kwa kipindi cha robo | - | - | - | - | (69,693) | - | (69,693) |
| Mapato mengine | | | | | | | - |
| Mtaji mkuu wa kisheria | | | - | | 67,005 | - | 67,005 |
| Tozo la Mali la mwaka jana | - | - | - | - | - | 434,618 | 434,618 |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | - | - | - | - | (54,944) | (54,944) |
| Gawio lililolipwa | | | | | | (272,551) | (272,551) |
| **Salio kwa Mwaka 31.12.2020** | **6,056,497** | **-** | **-** | **-** | **67,005** | **2,439,472** | **8,562,974** |
| **Salio la mwaka 01.01.2021** | **6,056,497** | **-** | **-** | **-** | **67,005** | **2,439,472** | **8,562,974** |
| Rekebisho : | - | | | | | | - |
| Akaunti zingine za Mtaji | - | | | | 62,118 | (67,004) | (4,886) |
| Toa: Mapato mengine | - | | | | | | - |
| Mtaji wa kisheria | - | | - | - | | | - |
| | - | | | | | | - |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | | | | | (207,855) | (207,855) |
| Toa: Gawio lililotolewa | - | | | | | - | - |
| **Salio kwa mwaka 31.12.2021** | **6,056,497** | **-** | **-** | **-** | **129,123** | **2,164,613** | **8,350,234** |

### ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2021

AINA YA BIDHAA

| 1. AKAUNTI ZA AKIBA | | | 2. Mkopo | |
|---|---|---|---|---|
| Kima cha chini cha kufun | 5000/= | | Mikopo ya biashara | 36% PA |
| Ada ya mwezi | BURE | | Mikopo ya kuboresha nyun | 18% PA |
| Taarifa ya Akaunti | BURE | | Ada ya Mkopo | 2.50% |
| Kuuliza salio | BURE | | Bima ya mkopo | 2.00% |
| Kufunga akaunti | 5000/= | | Mikopo ya Jikimu | 17% PA |
| Gharama za kuendesha | 5000/= | | Mikopo ya Kilimo | 30% PA |
| Gharama za kuweka fedh | BURE | | Mikopo ya Maji | 26% PA |
| | | | Mikopo ya wafanyakazi | 15% PA |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| **Imesainiwa na:** | **Cheo** | | **Tarehe:** |
|---|---|---|---|
| *Altemius Millinga* | *Mkurugenzi Mtendaji* | .............................. | *26-Januari-22* |
| *Samwel Gikaro* | *Meneja wa Fedha* | .............................. | *26-Januari-22* |
| *Humphrey Singogo* | *Kaimu Mkaguzi wa Ndani* | .............................. | *26-Januari-22* |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

**Kuthibitishwa na:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| *Ernest K. Ndimbo* | *Mwenyekiti wa Bodi* | .............................. | *26-Januari-22* |
| *Happy Sambega* | *Mkurugenzi* | .............................. | *26-Januari-22* |

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Takwimu za vifo, wagonjwa zitahamasisha chanjo corona

**SERIKALI** imeendeleza hatua za kuihamasisha jamii kujitokeza kupata chanjo ya ugonjwa wa UVIKO-19, baada ya kutamka kwamba kuanzia sasa itakuwa inatoa takwimu za wagonjwa na vifo vinavyotokana na ugonjwa huo.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, ndiye aliyetoa tamko aliyeangazia uamuzi huo mkoani Dar es Salaam juzi , akisema lengo ni kutaka kutambua umuhimu wa chanjo, ingawa ni hiari.

Ummy alisema hayo wakati wa kupokea chanjo 800,000 kutoka Serikali ya China, aina ya Sinopham ambayo itatumika kuchanja watu 400,000 dozi mbili.

Alisema hadi sasa chanjo zilizokwishapokelewa ni 8, 821,210 ambazo zinatosha kuchanja Watanzania, 5,082,380 na kwamba hadi juzi waliochanjwa ni 1,922,019 sawa na asilimia 3.33, tangu zilipoanza kutolewa mwaka jana aina ya Moderna, Jansen, Pfizer na Sinopham.

Alisema mwitikio wa kuchanja nchini bado ni mdogo wakati lengo ni kufikia asilimia 60 hadi mwishoni mwa mwaka huu.

Alisema ili kuongeza hamasa, kuanzia sasa serikali itakuwa inatoa takwimu za wagonjwa wanaougua na idadi ya vifo kutokana na ugonjwa huo, ili taarifa hizo zipimwe na jamii na kutambua umuhimu wa chanjo, ingawa bado serikali inasisitiza ni suala la hiari.

Ni ukweli usiopingika kwamba kasi ya Watanzania kuchanja ni ndogo kwa sababu asilimia 3.3 haiendani na muda ambao chanjo hiyo ilianza kutolewa nchini Julai mwaka jana.

Tunadhani kwamba taarifa mbalimbali za upotoshaji zilizokuwa zikitolewa ziliwafanya watu wengi kuamini kuwa ugonjwa huo hauko Tanzania sambamba na kuaminishwa kuwa chanjo ina madhara.

Suala lingine ambalo limechangia watu kusuasua katika kupata chanjo ni kutotolewa takwimu za vifo na wagonjwa, hivyo kuwafanya watu kutochukua hatua za tahadhari dhidi ya maambukizi.

Nchi nyingi zikiwamo za jirani zilianzisha utaratibu wa kutoa takwimu hizo kila siku, na hakika ilisaidia raia wake kuelewa kwamba kuna ugonjwa huo na watu wanaugua na wengine kufa.

Ingawa hata hivyo imechelewa, lakini tunaona kwamba serikali imefanya jambo hilo jema kwa lengo la kuijulisha jamii ukubwa wa tatizo za UVIKO-19 na hatua za kuchukua, ikiwamo kwenda kupata chanjo.

Katika moja ya nchi jirani, watu takribani milioni 10 walikuwa wamepata chanjo ya UVIKO-19, kwa mujibu wa takwimu za wiki mbili zilizopita, hali ambayo inadhihirisha kuwa utoaji wa takwimu unasaidia kuwahamasisha watu kuchanja.

Utaratibu wa utoaji takwimu za vifo na wagonjwa una lengo zuri la kuihamasisha jamii na si vinginevyo. Tunasema hivyo kwa kuwa kuna wanaoweza kupotosha kwamba kufanya hivyo ni kuwatia woga wananchi.

Tanzania sio kisiwa, hivyo inapaswa kushirikiana na mataifa mengine duniani katika masuala mbalimbali, ikiwamo mapambano dhidi ya ugonjwa huu ambao unaendelea kuleta majanga.

Kama alivyosema Waziri Ummy, bado kuna haja ya kuendelea kutolewa hamasa na elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa chanjo hii ili kufikia malengo ya kuchanja asilimia 60 ya Watanzania ifikapo mwishoni mwa mwaka huu. Viongozi wa serikali, taasisi na wa dini ni vizuri wakaendeleza hamasa kwa Watanzania kuchanja, ili kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Anthony Gervas, Mwanza

# Ajali hizi zitufunze pia kukabili karaha za wenzetu barabarani

**JAMANI** Watanzania wenzangu inauma kusikia ajali za huku na kule, tena baadhi zinatisha. Tujitahidi kuepuka ajali hizo zisizokuwa za lazima, uzembe, kuendesha mwendokasi, kutumia simu wakati dereva anaendesha gari, usingizi na unywaji pombe ni katika orodha ya yanayochangia ajali barabarani.

Ajali hizo watu wengi wamekuwa wakiziona kama vile za kawaida, kumbe zinapoteza maisha ya wengi wasio na hatia kila kukicha. Niseme kila kitu kina mwisho jamani! Ifikie mahali wananchi tupaze sauti zetu pamoja, ili tujinusuru kwenye mtego wa ajali za kila mara.

Utakuta dereva anaendesha basi la abiria safari ndefu kutoka mkoa kwenda mwingine anaongea na simu muda mrefu, gari liko mwendokasi halafu hataki kupunguza wala kumsikiliza abiria.

Wakati mwingine anaweza kuwa na usingizi au alikunywa pombe bado iko kichwani, baadaye anaweza kusababisha ajali hiyo ya watu kupoteza maisha bila ya sababu.

Serikali wakati ikipigana kupata dawa rasmi ya kuhakikisha inapata mbadala wa kudumu katika kudhibiti ajali hizo zisizokoma, ni busara sura ya ufumbuzi wa kudumu iwapo kwa kuanza na kuyaondoa magari mabovu barabarani.

Hilo linaendana na wahusika wa usalama barabarani kama Polisi Trafiki kuwawajibisha wote wanaokumbatia uzembe huo, ikiwamo kupokea rushwa za wakosaji barabarani.

Mimi nampongeza Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye kuitaka serikali kuchunguza ajali ya watu 14 waliofariki dunia katika wilaya ya Busega mkoani Simiyu.

Hapo iliwajumuisha wanahabari wenzetu wa hapa Mwanza waliokuwa wakielekea wilayani Ukerewe kikazi na abiria wanane waliokuwa basi dogo aina ya Toyota Hiace, pia dereva wa gari la serikali walilokuwamo manahabari watano.

Waziri Nnauye aliagiza polisi mkoani humo kuchunguza zaidi chanzo cha ajali hiyo na kutoa majibu, baada ya kushitushwa na ajali hiyo iliyotikisa Kanda ya Ziwa na Taifa, asubuhi saa 12:30 huko kijiji cha Shimanilwe wilayani Busega, baada ya gari la serikali kugongana uso kwa uso na hilo la abiria.

Ndugu wasomaji nawageukia wahusika wanaosimamia kitengo cha usalama barabarani (Trafiki), baadhi ambao huenda siyo waaminifu na wanasumbuliwa na pepo la kupokea rushwa, sababu mimi mwenyewe huwa napanda daladala na mabasi makubwa ya kusafiri na kuona mazingira nisiyokubaliana nayo.

Utashangaa pengine trafiki anasimamisha gari la daladala au basi kubwa la abiria, anapogundua lina makosa anazunguka nyuma yake na kumuita dereva au kondakta anayeshuka kumfuata, bila ya kujali ushuhuda fulani kutoka kwa abiria.

Baada ya hapo, anaendelea kukagua na baadaye anaruhusu gari liondoke, kukiwapo mazingira ya ukaguzi wenye kiulizo.

Sasa nawauliza enyi mnaolinda maisha yetu ya kila siku barabarani, baadhi yenu kuachia gari bovu katika mazingira hayo tata, hatujui tunaidhinisha mazingira ya ajali kwa gari hili bovu? Je,huo ni uungwana?

Hapa Mwanza nitoe kauli ya kuwakemea wenye pepo la rushwa waliepuke ili kunusuru maisha yetu Watanzania wana Mwanza. Nawaombeni mtumie busara na hekima, pia maadili ya kazi zenu.

Ndugu zetu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) naamini hili liko kwenye dhamana yenu kulichukulia hatua na ibaki simulizi.

Mtafanya vipi, jibu limo kwenye stadi zenu kikazi, pia mna nafasi ya kushirikiana kiutawala na mabosi wao hao wakosaji, muangalie namna gani mnaweza kulimaliza.

Nichangie kidogo tu. Takukuru nawafumbua macho hebu mthubutu kupanda daladala kwa siri na kushuhudia yanayotokea humo, niweke mfano wa Mwanza ninakopatikana, mjionee uhalisia unaotia karaha nafsi yangu huwenda na wengine.

Msisubiri mpaka kuletewa malalamiko au taarifa ofisini, nanyi jiongezeni. Huenda inaweza kufika pabaya watu wamenogewa na tabia, wanashindwa kuacha.

Tumeingia 2022, ugonjwa uleule na tabia ile ile ya mwaka jana inaendelea na huenda imekolezwa zaidi.

**TANGAZO**

# CITIBANK TANZANIA LIMITED

## Tanzu ya Citigroup, Kampuni iliyoshirikishwa nchini Marekani

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 31-Des-21 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30-Sep-21 |
|---|---|---|
| **A . MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 27,893 | 18,216 |
| 2 Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 149,152 | 60,230 |
| 3 Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 184,278 | 174,530 |
| 4 Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 374,053 | 154,758 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 145 | 173 |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7 Bili Zilizoafikiwa | 17,384 | 13,557 |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | 9,112 | 27,068 |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 46,100 | 168,261 |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 290,628 | 308,465 |
| 12 Mali Nyingine | 12,019 | 10,550 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| 14 Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 7,611 | 7,798 |
| 16 **JUMLA YA MALI** | **1,118,375** | **943,606** |
| **B . DHIMA** | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 793 | 785 |
| 18 Amana za Wateja | 885,020 | 619,328 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 Amana Maalumu | 9 | 9 |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2,412 | 2,489 |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3,566 | 3,042 |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 9,114 | 27,071 |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 792 | 736 |
| 27 Dhima Nyingine | 24,001 | 26,999 |
| 28 Madeni | 92,200 | 161,553 |
| 29 **JUMLA YA DHIMA** | **1,017,907** | **842,011** |
| 30 **MALI/(DHIMA) HALISI** | **100,468** | **101,595** |
| **C . FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 - Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 9,660 | 9,660 |
| 32 - Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 - Mapato Yaliyobakizwa | 81,736 | 81,553 |
| 34 - Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 6,346 | 6,878 |
| 35 - Akaunti Nyingine za Mtaji | 2,726 | 3,504 |
| 36 - Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| 37 **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **100,468** | **101,595** |
| 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 87,607 | 60,835 |
| 39 Mikopo Chechefu | 0 | 0 |
| 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,109 | 968 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | 0 | 0 |
| **D . BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| ( i ) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9.0% | 10.8% |
| ( ii ) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.0% | 0.0% |
| ( iii ) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 32.8% | 49.7% |
| ( iv ) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 26.0% | 32.7% |
| ( v ) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 75.9% | 67.6% |
| ( vi ) Ongezeko la Amana | 30.0% | -18.8% |
| ( vii ) Ongezeko la Mali | 15.6% | 3.9% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa 31-Des-21 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Des-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Des-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Des-20 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 7,826 | 6,823 | 30,978 | 31,303 |
| 2 Gharama za Riba | (1,906) | (2,375) | (7,739) | (12,192) |
| 3 **Mapato Halisi ya Riba** | **5,920** | **4,448** | **23,239** | **19,111** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (141) | 621 | (459) | 150 |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **4,197** | **3,951** | **14,473** | **13,468** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 3,017 | 2,789 | 9,486 | 8,822 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 1,180 | 1,133 | 4,987 | 4,616 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 0 | 29 | (1) | 29 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(8,768)** | **(7,056)** | **(26,225)** | **(25,360)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (2,787) | (2,329) | (9,502) | (7,975) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7.3 Gharama Nyingine | (5,981) | (4,727) | (16,724) | (17,385) |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,208** | **1,964** | **11,028** | **7,369** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (1,740) | (857) | (4,682) | (2,313) |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(532)** | **1,107** | **6,346** | **5,057** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | | | |
| Mapato ambayo hayajakamilika | (851) | 352 | 373 | 232 |
| Tengo la Kodi ya mapato ambayo hayajakamilika | 255 | (106) | (112) | (70) |
| Mapato mengine baada ya kodi ya mapato | (596) | 246 | 261 | 162 |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa** | **(1,128)** | **1,353** | **6,607** | **5,219** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 53 | 43 | 53 | 43 |
| 14 Mapato kwa Hisa | (53,184) | 110,635 | 634,577 | 505,650 |
| 15 Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **D . BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| ( i ) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.2% | 0.4% | 0.6% | 0.4% |
| ( ii ) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -2.1% | 4.5% | 6.4% | 5.2% |
| ( iii ) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 86.7% | 65.5% | 69.5% | 56.6% |
| ( iv ) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 4.2% | 3.8% | 3.4% | 3.4% |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

Imesainiwa na: Geofrey Mchangila (Ofisa Mtendaji Mkuu) — Date : 27 Januari 2022

Imesainiwa na: Iddi Msonga (Mkuu wa Fedha) — Date : 27 Januari 2022

Imesainiwa na: Godwin Rutashobya (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) — Date : 27 Januari 2022

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

Imesainiwa na: Andulile Mwakalyeye — Date : 27 Januari 2022

Imesainiwa na: Wilson Chola — Date : 27 Januari 2022

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya sasa 31-Des-21 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Des-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka 31-Des-20 |
|---|---|---|---|---|
| **I . Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 1,208 | 4,297 | 11,028 | 7,369 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| -Hasara Katika Mali | 518 | 536 | 1,947 | 2,546 |
| -Badiliko Halisi Katika Mikopo | 17,836 | (8,595) | 19,784 | (16,978) |
| -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (0) | 1 | 1 | (29) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Amana | 265,701 | (116,074) | (282,274) | 439,386 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | 0 | 0 | 0 | 0 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (20,108) | (7,809) | (33,024) | 22,017 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 12,916 | 7,349 | 17,740 | (25,470) |
| -Kodi Iliyolipwa | (2,084) | (605) | (3,983) | (2,703) |
| -Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **275,988** | **(120,900)** | **(268,781)** | **426,138** |
| **II . Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (330) | (298) | (681) | (2,601) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0 | 0 | 0 | 29 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (10,599) | 2,254 | (33,455) | 5,515 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(10,929)** | **1,956** | **(34,136)** | **2,943** |
| **III . Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (69,353) | 156,553 | 92,200 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | | | 0 | 0 |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(69,353)** | **156,553** | **92,200** | **0** |
| | **195,706** | **37,609** | **(210,717)** | **429,081** |
| **IV . Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **195,706** | **37,609** | **(210,717)** | **429,081** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 401,638 | 364,029 | 808,060 | 378,979 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 597,344 | 401,638 | 597,344 | 808,060 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | **9,660** | **0** | **85,916** | **1,582** | **0** | **1,759** | **98,917** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 6,346 | 0 | 0 | 0 | **6,346** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 261 | **261** |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Gawio lililolipwa/litakalolipwa | 0 | 0 | (5,057) | 0 | 0 | 0 | **(5,057)** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 877 | (877) | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **9,660** | **0** | **88,082** | **705** | **0** | **2,021** | **100,468** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | **9,660** | **0** | **92,611** | **0** | **0** | **1,597** | **103,868** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 5,057 | 0 | 0 | 0 | **5,057** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 162 | **162** |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Gawio lililolipwa/litakalolipwa | 0 | 0 | (10,170) | 0 | 0 | 0 | **(10,170)** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (1,582) | 1,582 | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **9,660** | **0** | **85,916** | **1,582** | **0** | **1,759** | **98,917** |

## CHARGES AND FEES- CITIBANK TANZANIA LIMITED

### CHARGES AND FEES- CITIBANK TANZANIA LIMITED

| 1.0 Current Accounts | CHARGE/FEE-LCY | CHARGE/FEE-FCY |
|---|---|---|
| (a) Required minimum opening balance | Waived | Waived |
| (b) Monthly service fee (breakdown per customer type) | TZS 20,000 | USD $20 |
| (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS 4,000 | US$ 5.00 |
| (d) Fees per ATM withdrawal | N/A | N/A |
| (e) ATM mini statement | N/A | N/A |
| (f) Interim statement per page | TZS 7,000 | US$ 5.00 |
| (g) Periodic scheduled statement | Waived | Waived |
| (h) Cheque book | TZS 35,000 (100 leaves) | US$ 35 (100 leaves) |
| (i) Dishonoured cheque | TZS 52,000 | US$ 50 |
| (j) Special clearance | TZS 60,000 | US$ 60 |
| (k) Counter cheque | TZS 2,500 per leaf | US$ 2 per leaf |
| (l) Stop Payment | TZS 30,000 | US$ 30 |
| (m) Standing order | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00<br>USD TISS: US $ 10.00 | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 USD TISS: US $ 10.00 |
| (n) Balance enquiry | Waived | Waived |
| (o) New ATM card issuance | N/A | N/A |
| (p) ATM card renewal or replacement | N/A | N/A |
| (q) Overdrawn account interest charge | 4.30%-7.55% | 1.38%-7.14% |
| (r) Unarranged overdraft | 15% | 10% |
| (s) Interbank transfer | Waived | Waived |
| (t) Bill payments through ATM | N/A | N/A |
| (u) Deposit fee | US $20 and below: 3% of deposited amount<br>TZS 1,000 and below: 0.3% of deposited amount<br>Coins: 3% of the deposited amount minimum TZS 10,000 | US $20 and below: 3% of deposited amount<br>TZS 1,000 and below: 0.3% of deposited amount<br>Coins: 3% of the deposited amount minimum TZS 10,000 |
| (v) Other (please specify) | N/A | N/A |
| (w) BRELA Search fees. Per search | TZS 30,000 | US$ 15 |
| (x) Foreign Loan Registration fees (DRN) | US$ 700 | US$ 700 |

| 2.0 Savings Accounts | | |
|---|---|---|
| (a) Required minimum opening balance | NA | NA |
| (b) Monthly service fee | NA | NA |
| (c) Interim statement | NA | NA |
| (d) Account clossure | NA | NA |

| 3.0 Electronic Banking | | |
|---|---|---|
| (a) Internet banking monthly fee | Waived | Waived |
| (b) Internet transfers | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00<br>USD TISS: US $ 10.00 | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.0 and Max US$ 500.00<br>USD TISS: US $ 10.00 |
| (c) SMS banking | N/A | N/A |
| (d) Other | Managers Cheques: TZS 4,000 | Managers Cheques: US$ 5.00 |

| 4.0 Foreign Exchange Transactions | CHARGE/FEE-LCY | CHARGE/FEE-FCY |
|---|---|---|
| (a) Purchase/sale of TCs transaction over the counter | NA | NA |
| (b) Purchase of foreign cheque | NA | NA |
| (c) Sale/purchase of cash passport | NA | NA |
| (d) Telegraphic transfer | | |
| -Inward Telegraphic Transfers [FTIN] | US$ 30 | US$ 30 |
| -Outward International TT / Electronic [ROCT] | 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 | 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 |
| (e) Telex/SWIFT | NA | NA |
| (f) Transfer from foreign currency denominated account to local current | NA | NA |

| 5.0 Personal Loans | | |
|---|---|---|
| (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | | |
| (i) Personal loans | NA | NA |
| (ii) Overdrafts | NA | NA |
| (iii) Mortgage finance | NA | NA |
| (iv) Asset finance | NA | NA |
| (b) Unpaid loan instalment | NA | NA |
| (c) Early repayment | NA | NA |
| (d) Valuation fees | NA | NA |
| (e) Other | NA | NA |

#### Additional Disclossures

| 1 Deposit Rates | LCY | FCY |
|---|---|---|
| -Current Account Deposits | 0%-3.00% | 0%-0% |
| -Time Deposits | | |
| (a) 1 - Months | -0.2%-0% | 0.07%-0.08% |
| (b) 3 - Months | 2.69% -2.99% | 0.18%-0.20% |
| (c) 6 - Months | 3.25% -3.55% | 0.30%-0.34% |
| (d) 9 - Months | 3.97% -4.27% | 0.41%-0.46% |
| (e) 12 - Months | 4.69% -4.99% | 0.52%-0.58% |

| 2 Lending Rate | LCY | FCY |
|---|---|---|
| Base lending rate | 9.05%-10.05% | 3.60%-4.60% |
| Short term ( up to one year ) | 9.05%-10.05% | 3.60%-4.60% |
| Medium term ( 2 to 3 years ) | 9.55%-10.55% | 4.10%-5.10% |
| Long term ( 3 - 5 years ) | 10.50%-11.05% | 4.60%-5.60% |
| Term loans ( over 5 years ) | 11.05%-12.05% | 5.10%-6.10% |

| 6.0 Trade Finance | CHARGE/FEE |
|---|---|
| **Documentary Collections** | |
| Imports | Handling: $130, Acceptance $65, Telex: 0.325% minimum $98 and maximum $650 |
| Exports | All in fee: $100 ($50 courier and $50 handling) per set of documents |
| **Imports Letters of Credits** | |
| Opening fees | LC issuance - 0.5% per quarter Min. $325 |
| Handling fees | Handling: $130 |
| Amendment Fees | Simple amendment $100, extension 0.5% per quarter if it extends to other quarter (s) |
| Confirmation fees | Confirmation 0.39% per quarter Min. EUR 390 per quarter |
| Risk margin on Acceptance | 0.25% per Quarter or part thereof |
| Other Bank LC re-issuance | 0.1% per Quarter, min. $200 |
| Bills Availization (Pour Aval) | 0.5% per Quarter or part thereof |
| **Exports Letters of Credits** | |
| Handling fees | $500 |
| Courier | $100 |
| Confirmation fees | 0.25% per Quarter or part thereof |
| Negotiation fees | 0.1% Min. $1000 |
| **Liquidity financing** | |
| Suppliers finance | Prevailing market rates and negotiable based on riskness of the transaction |
| Accounts Receivable Finance | Prevailing market rates and negotiable based on riskness of the transaction |
| **Guarantees and Standby Letters of Credits** | |
| SBLC | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Bid Bonds | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Performance Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Maintanance Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Advance Payment Guarantee | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Amendments fees on Guarantees | Simple amendments $100 and 0.5% per Quarter or part thereof, if it extends into next quarter(s) |
| Custom Bonds | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Warehouse Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Transit Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Facility fees | 1.5% per annum |

We the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information

| | Name | Designation | | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Iddi Msonga | CFO | ........................................................ | Date : 27th January 2022 |
| 2 | Michael Mungure | TTS Head | ........................................................ | Date : 27th January 2022 |
| 3 | James Rutta | Head of Treasury | ........................................................ | Date : 27th January 2022 |

# Wajawazito walia kukosa kituo cha afya

NA Pendo Thomas KIGOMA

WAJAWAZITO Kijiji cha Kamara, Kata ya Mgonya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, wanalazimika kutumia zaidi ya Sh. 50,000 kukodi gari kufuata huduma katika Kituo cha Afya Bitale na baadhi yao kujifungulia njiani au kupoteza maisha.

Wajawazito hao wamesema, kukosekana kwa kituo cha afya kwenye kata yao na jirani kunasababisha wanapopewa rufani kutoka zahanati ya Kamara kupata wakati mgumu kufika katika kituo hicho cha Bitale.

Pendo Michael, mkazi wa Kijiji cha Kamara, alisema wakati wa mchana kukodi gari kutoka eneo hilo gharama zake ni Sh. 50,000, lakini majira ya usiku hufika hadi Sh. 80,000.

Waliiomba serikali kusaidia uharakishwaji wa ujenzi wa kituo cha afya katika kata hiyo hatua itakayoondoa adha wanayoipata na kulinda afya ya mama na mtoto.

Monica Antony, mkazi wa eneo hilo alisema hali hiyo ina waathiri zaidi wananchi wenye kipato kidogo ambao baadhi yao hukosa fedha za kukodi gari kuwapeleka kilipo kituo cha afya.

"Kuna wakati tunalazimika kupitisha mchango ili mjamzito apate fedha za kukodi gari kwa kweli hii ni mbaya na ni tishio kwa usalama wetu," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Kamara, Omary Katura, alisema wananchi walichangishana na kufanikiwa kujenga msingi kwa zaidi ya miaka 10 iliyopita ambao hadi sasa ujenzi wake haujaendelea kutokana na kukosa fedha.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Lusajo Mwakajoka, alisema tayari wametenga bajeti ya Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Simbo jirani na Kata ya Mgonya.

Alisema kuanza kwa ujenzi huo kutategemea upitishwaji wa bajeti kutoka serikalini.

Kuhusu msingi wa kituo cha afya ulioanza kujengwa katika Kata ya Mgonya, alisema bajeti yake haipo kwa sasa hadi wakati mwingine itakapopitishwa.


A PRODUCT OF The Coca-Cola Company

KILIMANJARO DRINKING WATER

TAARIFA KWA UMMA

**BONITE BOTTLERS LTD** inapenda kuufahamisha umma juu ya kusitisha matumizi ya **plastiki laini (seal)** katika vifuniko vya chupa za **Maji ya Kilimanjaro** kutokana na agizo la serikali juu ya matumizi ya plastiki hizi kulinda mazingira.




@kilimanjaro_drinking_water kilimanjarodrinkingwater kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422


## Mil. 100/- kujenga vibanda vya machinga

Na Christina Haule, MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro inatarajia kutumia Sh. milioni 80 hadi 100 katika kukamilisha ujenzi wa zaidi ya vibanda 150 vya wafanyabiashara wadogo (machinga) katika eneo la Fire.

Mhandisi wa Manispaa ya Morogoro, Juma Gwisu, alisema hayo jana wakati kamati ya fedha ya Manispaa ilipotembelea eneo la ujenzi kuangalia maendeleo ya kazi hiyo.

Alisema baada ya kukamilika kwa vibanda hivyo, wajasiriamali wadogo watavitumia kufanya biashara zao na kwamba watakuwa katika mazingira rafiki ya kibiashara.

"Mpaka sasa tumekamilisha vibanda 88. Lengo letu na mpango wetu ni kujenga vibanda 150, lakini tutahakikisha tunakamilisha kwa wakati vibanda vilivyobaki ili wafanyabiashara waanze biashara na kufanya kazi katika mazingira rafiki," alisema Gwisu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha Manispaa ya Morogoro, Paschal Kihanga, alisema ujenzi huo ni mwendelezo wa ujenzi wa vibanda vya wafanyabiashara wadogo katika manispaa kama vilivyojengwa kwenye soko la Chifu Kingalu mwaka jana.

Alisema lengo la kujenga vibanda hivyo ni kuwakusanya wafanyabiashara mahali pamoja na kuondokana na msongamano maeneo ya pembezoni mwa barabara.

Kihanga alisema msongamano wa wafanyabiashara wadogo pembezoni mwa barabara, mara nyingi umekuwa ukitishia hata uhai wao na wanunuzi wanaopita kwenye maeneo yao kutokana na kufanya biashara kwenye eneo dogo.

Mmoja wa wafanyabiashara wa eneo moja la barabara za manispaa, Flora Msangi aliishukuru manispaa kwa kuona umuhimu wa kuwajengea eneo maalum ambalo watalitumia kufanya biashara zao.

Morogoro ni miongoni mwa manispaa zilizofanya vizuri katika ujenzi wa vibanda vya machinga na kuwa ya mfano ya kujifunza ujenzi wa vibanda hivyo kwa kutekeleza ujenzi wa vibanda vya machinga katika Soko Kuu la Chifu Kingalu katika mpango uliosimamiwa na kuendeshwa na Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando.

## TRA yavuka lengo makusanyo ya kodi

Na Richard Makore, MWANZA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Mwanza, imevuka malengo ya makusanyo ya lengo lililojiwekea katika kipindi cha nusu mwaka 2021/22 kwa kukusanya Sh. bilioni 32 badala ya Sh. bilioni 28.7.

Pia mamlaka hiyo katika kipindi cha nusu mwaka kati ya Julai hadi Desemba 2021, imekusanya Sh. bilioni 106.4 kati ya Sh. bilioni 113 iliyopangwa katika muda huo.

Meneja wa TRA Mkoa wa Mwanza, Joseph Mtanda, alisema jana kuwa katika kipindi cha miezi sita ambacho ni nusu mwaka, kodi ya ushuru na forodha imefanya vizuri na kuvuka lengo.

Alisema ushuru unaotozwa kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi, umeongezeka na kwamba mamlaka hiyo itaendelea kuweka mkazo katika eneo hilo.

Kuhusu makusanyo ya kodi za ndani, Mtanda alisema katika kipindi hicho cha nusu mwaka, wamekusanya Sh. bilioni 73.7 sawa na utendaji wa asilimia 87.

Akizungumzia makusanyo ya jumla katika kipindi hicho, Mtanda alisema mapato yameongezeka na kwamba katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21, walikusanya Sh. bilioni 90 kati ya lengo la Sh. bilioni 100.7 walilokuwa wamejiwekea.

Hata hivyo, Mtanda alisema kodi ya ongezeka la thamani (VAT) bado inasumbua kwa kuwa watu hawana utamaduni wa kudai risiti wanaponunua bidhaa na wafanyabiashara nao hawatoi risiti.

Alisema kuanzia Februari Mosi, mwaka huu, atakayebainika kutodai risiti, akikamatwa atafikishwa mahakamani na endapo atapatikana na hatia, atahukumiwa faini ya kuanzia Sh. 30,000 hadi Sh. milioni moja na kwa mfanyabiashara atayeshindwa kutoa risiti, adhabu yake itakuwa kati ya Sh. milioni tatu hadi 4.5.

Meneja huyo aliwataka wananchi kujenga utamaduni wa kudai risiti kwa kila bidhaa wanayonunua na wafanyabiashara na wao wahakikishe wanafuata sheria kwa kutoa risiti halali.

Mwanza ni miongoni mwa mikoa minne nchini ambayo inafanya vizuri katika makusanyo ya kodi za serikali.

# ZLB yapewa kongole kwa kusimamia sheria ya vileo

**Na Mwandishi Wetu**, ZANZIBAR

BODI ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar (ZLB), imepongezwa kwa kuteua kampuni tatu za kuingiza vileo Zanzibar kati ya tisa zilizojitokeza baada ya kushinda zabuni kwa mujibu wa kifungu cha Sheria Namba 33(1) cha Sheria ya Vileo Namba 9 ya Mwaka 2020.

Mwanaharakati wa Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ali Makame Issa, aliipongeza Bodi hiyo alipozungumza na Waandishi wa Habari, mjini hapa siku moja baada ya Mwenyekiti wa Bodi, Khamis Haji, kutangaza kampuni zilizochaguliwa kuingiza vileo katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Issa alisema utaratibu wa kisheria wa kuweka kampuni tatu kuingiza vileo utasadia kudhibiti mapato ya serikali na kuweka mfumo mzuri wa uendeshaji wa biashara hiyo visiwani humo.

"Bodi mpya ya vileo inapaswa kupongezwa imeanza kazi vizuri kwa kusimamia sheria kama ilivyotungwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi na kuanza kutumika baada ya kusainiwa na Rais wa Zanzibar," alisema Issa.

Alisema kwa mujibu wa kifungu cha Sheria Namba 33(1) cha Sheria Namba 9 ya vileo ya mwaka 2020 imesema kampuni za uingizaji vileo zinatakiwa kuwa tatu na mmiliki lazima awe Mzanzibari mlipa kodi na awe na ghala na gari za kusambazia vinywaji.

"Kwa kweli tunampongeza Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hatua ya kuvunja Bodi ya zamani na kuunda mpya. Bodi mpya imeonyesha uwezo wa kusimamia sheria," alisema Issa.

Alisema wananchi wa Zanzibar wamepata faraja kubwa jinsi awamu ya nane inavyosimamia sheria na kufuata misingi ya utawala bora na kuwataka wananchi waendelee kuunga mkono juhudi za Rais Dk. Mwinyi katika mpango wa kukuza uchumi wa buluu unaolenga kutumia rasilimali za baharini.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi, alisema hatua ya kuchagua kampuni tatu za uagizaji wa vileo imezingatia sheria ya kudhibiti, kusimamia uagizaji, uhifadhi, uuzaji, usambazaji na unywaji wa vileo Zanzibar.

Alitaja kampuni zilizo chaguliwa ni One Stop, Scoch Limited na Zanzibar Maritime Mercantile Limited baada ya kukidhi viwango na masharti kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa kifungu cha 33 (2) cha sheria ya vileo mtu yeyote atakaeagiza vileo bila ya kibali ni kosa la jinai na adhabu yake ni kifungo cha miaka miwili au faini ya Shilingi milioni tatu na vileo kutaifishwa au adhabu zote.

Alisema Kampuni hizo tatu zimeteuliwa baada ya kukamilisha matakwa ya sheria na kulipia gharama za ukaguzi Shilingi milioni tano na kibali Shilingi milioni 30 na mwisho wa kutumika ni Desemba, mwaka huu.

Akitangaza kanuni za ada za leseni, alisema fomu za baa na ada yake Sh. 400, 000, ukaguzi Sh. 300,000, leseni Shilingi milioni tatu, wakati maduka yanayouza pombe fomu moja Sh. 400,000, ukaguzi Sh. 300,000 na leseni Sh. milioni 2.5 kwa mwaka.

Alisema Bodi ya Udhibiti wa Vileo imejipanga kuhakikisha sheria inatekelezwa kama ilivyopitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar (BLW) iliyokuwa ikitumika kuanzia Mei 11, 2020 baada ya kusainiwa na Rais mstaafu Dk. Ali Mohamed Shein.



Baadhi ya wanachama wa Chama cha Wachimbaji Madini Wanawake Tanzania (TAWOMA), wakionyesha bidhaa za madini wakati wa mkutano wao mkuu, ulidhaminiwa na Barrick Gold Corporation, jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kattanga akunwa ubora huduma mahakama

**Na Mary Gwera**, DODOMA

KATIBU Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Kattanga, ameipongeza mahakama kwa uboreshaji wa huduma na kushauri kuhusisha wanafunzi katika matukio mbalimbali ili kuwapa hamasa ya kuipenda fani ya sheria.

Balozi Kattanga alisema hayo juzi alipotembelea mabanda ya Maonesho ya Wiki ya Sheria nchini yanayofanyika kitaifa katika Viwanja vya Nyerere 'Square' jijini Dodoma.

Akizungumza baada ya kukagua mabanda kadhaa, Balozi Kattanga alisema amefurahi kuwa Mahakama imepiga hatua katika uboreshaji wa huduma mbalimbali zinazotolewa.

"Nina furaha kuwa katika kipindi cha takribani miaka mitatu niliyotoka mahakamani, naona kuna mabadiliko makubwa ambayo yametokea hususani upande wa mifumo ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano). Naomba utaratibu wa kuwahusisha wanafunzi wa shule mbalimbali uendelee ili kuwajengea uwezo wa kuipenda fani ya sheria mapema," alisema.

Balozi Kattanga aliahidi kuwa serikali itaendelea kutoa ushirikiano wa mhimili wa Mahakama ili kuuwezesha kuendelea kutoa haki kwa wananchi.

Katika ziara hiyo, Balozi Kattanga alitembelea Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki (IJC), Dodoma na kukagua mradi wa ujenzi wa makao makuu ya Mahakama ya Tanzania katika eneo la Tambuka Reli jijini hapa.

Alionyesha kufurahishwa na ubora wa jengo la IJC Dodoma na hatua kubwa iliyofikiwa ya mradi wa ujenzi wa makao makuu ya Mahakama.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Prof. Elisante Ole Gabriel, alimshukuru Katibu Mkuu Kiongozi kwa kutenga muda na kutembelea maonyesho hayo, kutembelea jengo la IJC na kukagua mradi wa ujenzi wa makao makuu ya Mahakama.

"Nikiri wazi kuwa nimefurahishwa na ujio wako Mhe. Balozi Kattanga na tunashukuru kwa ushirikiano ambao serikali inaendelea kutupa, kutuwezesha kutimiza malengo yetu. Tunaahidi kuendelea kuboresha huduma na kuendeleza mazuri yote uliyoyaacha ukiwa mtendaji mkuu wa Mahakama," alisema Prof. Ole Gabriel.

# Tanzania kuendelea kuimarisha uhusiano wake mataifa ya nje

**Na Maulid Mmbaga**

TANZANIA imezidi kuimarisha ushirikiano na mataifa mbalimbali duniani zikiwamo nchi za Morocco, India na Oman katika kujiongezea maarifa, uzoefu na kujiimarisha kibiashara na kijamii ili kuleta maendeleo na kuinua uchumi wa taifa.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula na Waziri wa Mambo ya Nje wa Morocco, Nasser Bourita, walisema hayo walipofanya mkutano kwa njia ya mtandao jana na kukubaliana kushirikiana katika nyanja za biashara, uwekezaji, elimu, utalii na uwezeshaji wa kiuchumi kwa wanawake na vijana.

Balozi Mulamula alisema walizungumzia masuala ya kuimarisha uhusiano kati ya Tanzania na Morocco na kupitia makubaliano yaliyofikiwa wakati wa ziara ya Mfalme wa nchi hiyo alipotembelea Tanzania mwaka 2016.

"Tumepitia mikataba mbalimbali iliyotiwa saini wakati wa ziara hiyo, lakini pia tumejadili umuhimu wa kuwa na tume ya pamoja ya ushirikiano," alisema Mulamula. Vilevile, walijadiliana na kukubaliana kuimarisha ushirikiano wa karibu katika sekta za biashara na uwekezaji, utalii, elimu hasa katika kuongeza idadi ya ufadhili wa masomo kwa Watanzania kutoka wanafunzi 30 hadi 50.

"Morocco ni nchi inayopata watalii wengi, hivyo tumekubaliana kushirikiana kwa karibu zaidi ili kupata uzoefu ni njia gani wanatumia kukuza sekta ya utalii," alisema Mulamula.

**INDIA**

Balozi Mulamula pia alishiriki sherehe za maadhimisho ya 73 ya Jamhuri ya India zilizofanyika jijini Dar es Salaam, na kusema Tanzania na India zimeahidi kuongeza maeneo mapya ya ushirikiano ili kuleta maendeleo endelevu kwa maslahi ya pande zote mbili.

Alisema nchi hizo zimedhamiria kufanya kazi kwa karibu katika kutafuta njia bora ya kufungua na kuimarisha fursa mpya za biashara na uwekezaji zilizopo kati ya nchi hizo.

"Kuanza kwa safari za ndege za moja kwa moja kutoka Dar es Salaam hadi Mumbai kwa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) na kufunguliwa kwa soko la parachichi nchini India ni miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ili kuimarisha na kukuza uhusiano wetu katika sekta za biashara na uwekezaji pamoja na utalii kati ya nchi hizo," alisema Balozi Mulamula.

Pia, alibainisha kuwa Tanzania na India kwa sasa zimeanzisha ushirikiano katika usambazaji wa nishati, ujenzi wa miundombinu na kilimo.

"Uwekezaji wa India pamoja na idadi ya raia wake wanaotembelea Tanzania kwa madhumuni ya kuwekeza katika sekta za madini, utalii, viwanda, kilimo, usindikaji wa mazao ya kilimo, nishati, usafirishaji, ujenzi, huduma za fedha na maendeleo ya rasilimali watu unaendelea kuongezeka kwa kasi," alisema.

Kwa upande wake, Balozi wa India nchini, Binaya Srikanta Pradhan, alisema Tanzania imekuwa na uhusiano mzuri na nchi yake ambayo ni chachu ya maendeleo kwa mataifa yote mawili na kusababisha kuongeza maeneo mapya ya ushirikiano.

"Ushirikiano na mshikamano uliopo baina ya mataifa yetu mawili umekuwa chachu ya maendeleo na lengo la ushirikiano wetu ni kukuza uchumi wetu," alisisitiza Pradhan.

Balozi Pradhan pia alisema Tanzania itaendelea kuwa ya kipekee kwa taifa la India kutokana na mshikamano ambao umesababisha mataifa hayo kufanya biashara, uwekezaji, kujenga uwezo, ujenzi wa miundombinu pamoja na maendeleo ya kiuchumi.

**OMAN**

Katika tukio lingine, alikutana na kufanya mazungumzo na Kaimu Balozi wa Oman nchini Dk. Salim Saif Al Harbi jijini Dar es Salaam na kujadiliana masuala mbalimbali ya kuendeleza na kuimarisha ushirikiano uliopo kati ya nchi hizo mbili.

# Wafundwa kufanya kazi kibiashara zaidi

Na Mwandishi Wetu

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Tixon Nzunda, ameielekeza Wakala wa Maabara ya Veterinari nchini (TVLA) kufanya kazi kibiashara ili iweze kujiendesha yenyewe bila kutegemea ruzuku kutoka serikalini.

Nzunda aliyasema hayo juzi alipofanya ziara yake ya kwanza tangu alipoteuliwa kushika wadhifa huo Januari 8, 2022.

"Fanyeni kazi kibiashara na kwa uadilifu mkubwa, mashamba ya mifugo yanayovamiwa na wananchi hakikisheni mnayatumia kibiashara kwa kutenga fedha kwenye bajeti yenu ili yaweze kupimwa ili kuondokana na adha ya kuvamiwa na wananchi," alisema Nzunda.

Mbali na suala la kuimarisha mashamba ya mifugo, Nzunda alielekeza mifumo ya utendaji kazi ya kielektroniki iimarishwe katika vituo vyote vya wakala hiyo.

Akielezea kuhusu changamoto ya uhaba wa watumishi wa wakala hiyo, Nzunda amemuelekeza Mtendaji Mkuu wa Wakala hiyo kufuatilia maombi ya kuajiri watumishi wapya Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma ili kukidhi mahitaji ya taasisi hiyo.

Vile vile, Nzunda ameelekeza kulindwa na kutunzwa kwa mali za wakala hiyo ili ziweze kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Pia, ameelekeza Wakala kufanya kazi kwa karibu na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) cha Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kutangaza kazi zao.

Aliielekeza Wakala hiyo kukutana na wadau wanaotumia chanjo hizo kila mwaka ili kupata mrejesho kutoka kwa wadau hao.

Aliitaka Wakala ijikite katika kutafuta masoko ya chanjo hizo nje na ndani ya nchi. Awali, akisoma taarifa fupi ya Wakala hiyo, Mtendaji Mkuu wa Wakala hiyo, Dk. Stela Bitanyi, alibainisha kuwa kazi kubwa wanayofanya ni uchunguzi na utambuzi wa magonjwa ya wanyama na wadudu wanaosambaza magonjwa na uhakiki wa usalama na ubora wa vyakula vya mifugo.

Dk. Stela alisema Wakala inatimiza majukumu yake kwa kupima, kutathmini na kuhakiki vitendanishi, mimea tiba pamoja na kemikali zinazotumika katika maabara za wanyama.

Dk. Bitanyi aliongeza kuwa Wakala hiyo kupitia Taasisi ya Chanjo nchini (TVI) inatengeneza na kuzalisha aina saba za chanjo dhidi ya magonjwa ya mifugo ikiwa ni pamoja vitendanishi.

"Chanjo za mifugo zinazozalishwa na TVLA ni pamoja na Temevac(chanjo dhidi ya mdondo), Kimeta, Chambavu,Tecoblax (mchanganyiko wa Kimeta na Chambavu), kutupa mimba (Brucellosis), homa ya mapafu ya ng'ombe (CBPP) na homa ya mapafu ya mbuzi (CCPP)," alisema Dk. Bitanyi. Alisema kuwa ili kusogeza huduma karibu kwa wafugaji, vituo hivyo vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo vipo pia katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Mtwara, Mwanza, Sumbawanga, Tabora na Kliniki ya Mifugo na Maabara Meatu-Simiyu.

Katika ziara hiyo Nzunda pia alitembelea kiwanda cha kuzalisha Chanjo Kibaha (TVI) na kujionea jinsi chanjo za mifugo zinavyotengenezwa na kuwataka wanasayansi hao kuongeza umahiri na weledi katika kazi zao na kuzingatia uadilifu.

# Mnada kidijitali TFS waingiza bil. 1.3/-

Na Mwandishi Wetu, TANGA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) jana ilifanya mnada wa miti aina ya misaji kwa njia ya kielektroniki na kuuza vitalu vyote 10 ilivyotangaza kuviuza katika mashamba ya Longuza mkoani Tanga na Mtibwa, Morogoro na kupata zaidi ya Sh. bilioni 1.3.

Kamishina Msaidizi Mwandamizi wa TFS anayesimamia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Harold Chinpanha, alisema mfumo huo unapatikana katika njia ya tovuti na 'MobileApp' unawawezesha wateja kushiriki mnada pamoja na watumishi wa wakala kufuatilia mchakato mzima.

"Hii ni mara ya kwanza kwa TFS kuendesha mnada kwa njia ya kielektroniki kwa kutumia mfumo uliobuniwa na kutengenezwa na wataalamu wa ndani wa TEHAMA wa wakala. Kupitia mfumo huu, tumeuza kwa asilimia 100 miti yote iliyopimwa katika mashamba ya Mtibwa na Longuza.

"Awali tulitarajia kukusanya Sh. 1,041,827,580 kwa bei ya kuanzia na baada ya kuuza tunatarajia kukusanya maduhuli ya serikali zaidi ya Sh. bilioni 1.3. kati ya fedha hizo Sh. 575,636,252 tumeuza katika shamba la Mtibwa huku Longuza tukiingiza Sh. 748,982,951.50 hii ni sawa na asilimia 127," alisema Chinpanha.

Fedha hizo, alisema zimepatikana baada ya kuuza mita 1,963,331 za ujazo za miti hiyo. Mita 1,144.038 ziliuzwa Mtibwa na 819.293 shamba la Longuza.

Chipanha alisema TFS inatambua TEHAMA ndipo dunia ilipo na inakoelekea, hivyo kuanzishwa kwa mauzo ya mnada kwa njia ya kielektroniki kunalaenga kuachana na utaratibu wa kuuza katika ofisi za mashamba husika ili kuongeza uwazi na ushindani.

Daniel Silima, Kamishina Msaidizi Mwandamizi anayesimamia Leseni, alisema kampuni zote zilizoshinda zabuni hiyo, zinatakiwa kulipa asilimia 25 ya thamani yote ndani ya siku tatu za kazi kuanzia siku ya mnada.

Alisema Fedha hizo hazitarudishwa endapo mshindi atashindwa kulipia ujazo aliouziwa.

"Licha ya mnada huu kuwa wa kielektroniki, kanuni za mnada zinabaki kama zilivyo. Tayari tumeshawapa hati ya madai ya mfumo wa kielektroniki wa makusanyo ya serikali (GePG) wanunuzi wote. Asilimia 75 iliyobaki watalipa ndani ya siku 14 baada ya mnada," alisema Salima.

Mwanasheria wa TFS, Salome Rwiza, alisema mnunuzi aliyeshinda mnada, atatakiwa kuondoa mazao aliyonunua ndani ya miezi miwili baada ya kumaliza kulipa malipo yote yanayostahili.



Meneja Afya, Usalama na Mazingira wa Kampuni ya bia ya Serengeti (SBL), Simon Peter (kushoto), akifafanua jambo kwa wanafunzi wanufaika wa programu ya Kilimo Viwanda inayotolewa wa kampuni hiyo, pamoja na wakuu wa vyuo wanavyosoma walipotembelea kiwanda cha SBL cha Dar es Salaam jana. Habari Uk. 24. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Pakistan yaialika Tanzania maonyesho ya bidhaa

Na Maulid Mmbaga

MAMLAKA ya Maendeleo ya Biashara nchini Pakistan (TDAP) na sekta binafsi nchini humo, wameandaa maonyesho maalum ya vifaa vya uhandisi na afya yatakayoshirikisha Afrika na Jamhuri za Asia ya Kati yatakayofanyika Lahore nchini humo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na ubalozi wa Pakistan nchini, maonyesho hayo yatafanyika kuanzia Februari 25 hadi 27 mwaka huu, yakihusisha bidhaa nzito, za kati na nyepesi za uhandisi na huduma ya afya ikiwamo dawa, vifaa vya tiba na upasuaji.

"Wafanyabiashara, wanunuzi wakubwa wa nyumba, maduka ya minyororo, mashirika ya biashara, wawakilishi wa mashirika ya kukuza biashara na mamlaka za udhibiti za serikali zikiwamo kutoka Afrika Mashariki na Tanzania wanatarajiwa kuhudhuria maonyesho hayo," ilisema.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa miongoni mwa bidhaa kubwa zitakazoonyeshwa katika maonyesho hayo ni pamoja na mashine na zana za kilimo, za umeme aina zote, vifaa vya ujenzi, bidhaa za chuma na vifaa vya usalama ikiwamo madini.

Bidhaa zingine ni magari ya tingatinga na malori, kemikali, marumaru, simu za mkononi, vipandikizi, vifaa vya kupikia, karatasi, vifaa vya mpira, vyombo vya plastiki, samani, mavazi, vyombo vya muziki, vipodozi na vito.

"Zaidi ya waonyeshaji 250 wa nchini Pakistan na wawakilishi wakuu kutoka mashirika husika ya kibiashara watakuwa wakiandaa maonyesho hayo. TDAP pia itapanga ziara za kiwandani kwa wanunuzi wa kigeni kama ufuatiliaji wa mikutano wakati wa maonyesho hayo," ilisema.

Alisema washiriki kutoka Tanzania na ukanda mzima wa Afrika Mashariki watakaovutiwa kushiriki maonyesho hayo, wanaweza kusajili ushiriki wao kwenye tovuti maalumu ya mtandaoni ambayo ni https://ehcs.tdap.gov.pk




Ukurasa 13

Watanzania tupalilie uchifu wa kisasa tu



**Uongozi Dar wafunguka undani ubishi wa Machinga dhidi ya agizo waondoke**

Ukurasa 14


# BUFE

IJUMAA JANUARI 28, 2022

**BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA**

Nipashe


JICHO LA TATU LA RAIS SAMIA;

# Mbinu mkakati Utambulisho Mikoa utakavyochochea maendeleo kitaifa

## • Utamaduni wa tamasha kubeba jukumu

**Na Mwandishi Wetu**




Rais Samia Suluhu Hassan, alipokuwa mgeni rasmi kwenye Tamasha la Utamaduni jijini Mwanza. **PICHA: MTANDAO.**

MTU anaporudishwa shule darasa la Jiografia, tena shule ya msingi anakumbushwa ramani ya Tanzania yenye ukubwa kilometa za mraba 945,087 ndani yake kukiwapo na mikoa 31.

Pia, akirejeshwa katika masomo ya Uraia na Historia, kunapatikana dondoo; utulivu na amani ndiyo nguzo yake, kukiwapo orodha ya waasisi waliotangulia mbele ya haki.

Katika majivuno hayo ya haki, jamii inawajibishwa ulinzi na utetezi wa utamaduni wake, ikiwa sehemu ya kudumisha umoja huo.

Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye kwa sasa ameshika dhamana ya uongozi wa nchi tayari yuko katika safari anayozidi kuvuta mapinduzi ya safari ya uchumi na maendeleo na si ajabu kumbashiria 'hapati usingizi' kwa hilo.

Dira yake ni mapinduzi ya fikra hasa kwa vijana wanaokaribia theluthi mbili ya Watanzania wote, wahame kutoka maisha ya utegemezi.

Tanzania hadi sasa inajipanga kwa maboresho ya uchumi wa ndani, huku nje yake kukiwapo mapambano ya kumiliki masoko ya pamoja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), dunia ya utandawazi na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda.

**UTAMBULISHO WA MIKOA**

Hivi sasa Rais Samia, mbali na kutaka watendaji kitaifa kutaka wasaidizi wake kusaka na kuvuna fursa zilizoko ndani ya EAC na nyayo zote duniani za diplomasia ya uchumi, pia ndani ya mipaka ana lake la ziada analoliita 'utambulisho wa mikoa.'

Msingi wake, Rais Samia, anaiona mikoa imejaa fursa na sasa anataka ziundiwe utambulisho wake maarufu 'regional branding' utakaozisaidia kujenga uchumi wake na kitaifa.

Msingi wa utambulisho ni dhana pana inayohitaji dhamira ya dhati kutoka kwa viongozi, pia wananchi husika kwa pamoja.

Utambulisho mkoa unatajwa kuwa uti wa mgongo wa eneo husika katika kuinua uchumi wake, ikitambulisha na kuonyesha fursa zilizopo, zikiambatanishwa na kiini kikuu cha utamaduni wa wenyeji na sehemu husika.

Hapo ndipo kunaiwezesha serikali kugawa fursa za maendeleo kutokana na utambulisho huo husika, mathalani inakuwa ngumu kujenga kiwanda cha kuchakata nyama Singida, iwapo mkoa huo unahitaji pembejeo za kilimo cha alizeti,

Kinadharia, inafafanuliwa taifa imara huzaliwa kwenye utamaduni madhubuti unaolinda soko lake na sio chanzo mbadala.

Mara zote inajulikana kiu ya dunia huwa ni kuujua utamaduni wa Afrika, huku nchini Tanzania, Rais Samia anawekeza zaidi ikiwamo kupitia ushiriki wake kwenye matamasha ya utamaduni, mfano mkoani Mwanza na Kilimanjaro hivi karibuni.

Rais ameanika bayana kuwa umuhimu wa nchi kusimamia na kuhamasisha ushiriki wa vijana katika shughuli halali za kijamii na kiuchumi katika maeneo waliko, akihimiza mabadiliko ya kifikra, dhana na mitazamo ambayo mara nyingi inawazuia vijana kuchangamkia na kutumia fursa zao.

Pia, anataja haja ya kupashana taarifa za fursa zilizopo na zijazo ndani na nje ya nchi, ili kuandaa mazingira na utayari wa kunufaika nazo, mfano ukielekezwa kwenye uwezekano wa mabadiliko ya hali ya hewa, yanayoathiri mpangilio wa wanyama hifadhini, mbadala ukiangukia Utalii wa Utamaduni.

Rais Samia anahimiza haja ya kuwaona vijana wanashirikiana kwa kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu, hata kujengeana uwezo unaochochea ukuaji biashara, sanaa na mengine ya maendeleo.

Hata hivyo, anataja vigezo vya kuwanyanyua vinajumuisha miundombinu wezeshi kwenye biashara, urahisi wa kupatikana mitaji, unafuu wa kodi, ada na tozo, pia sera na sheria rafiki kwa vijana, hususani wajasiriamali wadogo na kati.

**DARASA LA UGHAIBUNI**

Mtu anapokanyaga ndani ya taifa kubwa Marekani, anakutana na matamasha makubwa ya sanaa na muziki kama Coachella na Sherehe za Kwanza, zote zikiwa sehemu ya utambulisho wa maeneo hayo.

Ni matamasha yaliyojengewa misingi ya utamaduni, ambao baadaye unabadilika kuwa fursa kwenye maisha ya vijana na mwisho wa safari, nchi ya Mare-

**INAENDELEA UK 12**

UCHUMI

MENEJA WA TPA ZIWA TANGANYIKA:

# Bandari ya Karema rasmi Machi ijayo, hofu iliyobaki kwetu barabara mbovu

- Wenyeji Katavi, mikoa jirani kufunguka kiuchumi
- Burundi, DRC na Zambia mbadala wa Tunduma
- Wazawa 300 wachekelea ajira ya miaka miwili

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa Mpanda**

MRADI wa ujenzi wa bandari ya Karema unatekelezwa katika mwambao wa Ziwa Tanganyika, ikiwa ni umbali wa kilometa 120 za barabara ya vumbi kutoka Wilaya ya Mpanda, mkoani Katavi.

Ujenzi wa bandari hiyo unagharimu Sh bilioni 47.97, ikiwa na gati lenye urefu wa mita 150 inayoweza kuhudumia meli zenye urefu wa mita 75 kila moja kwa wakati na ina kina cha mita 4.5.

Ni eneo ambalo kitaalamu linatajwa kufikika kirahisi na vyombo mbalimbali vya majini vinavyofanya biashara katika maeneo ya jirani na bandari pamoja na nchi jirani za Burundi, Zambia na DRC.

Kukamilika kwa mradi huo kunatarajiwa mwezi Machi mwakani kwa dira ya kusaidia kwa kiasi kikubwa kufunguka uchumi kwa wananchi, mikoa jirani na hata nchi za jirani zinazotegemea bidhaa kutoka Tanzania.

Kaimu Meneja wa Bandari Ziwa Tanganyika, Manga Gasaya, anasema mradi wa ujenzi wa bandari hiyo unatekelezwa na kampuni ya ujenzi ya Kichina iliyoingia mkataba na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) Agosti 3 mwaka 2019 kwa gharama ya Sh bilioni 47.97.

Anasema utekelezaji huo wa mradi kwa muda wa miezi 24 au miaka miwili, ulianza Oktoba 25 mwaka 2019 na unatarajiwa kukamilika Machi 6 mwakani.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alipozulu kukagua ujenzi wa Bandari ya Karema, mkoani Katavi, mwaka uliopita.

Gasaya anasema kazi zote za awali zinasaidia ujenzi wa miundombinu ya kudumu ya bandari ya Karema kama vile usanifu yakinifu, maandalizi ya eneo la mradi, maabara ya mradi, uwekaji mtambo wa kuchanganya zege, uingizaji mitambo ya ujenzi katika eneo la mradi na utafiti wa malighafi za ujenzi umekamilika kwa asilimia 100.

"Kwa ujumla mradi wa ujenzi wa bandari ya Karema umefikia asilimia 66 ya utekelezaji wake na jumla ya Shilingi bilioni 19.4 zimeshalipwa kwa mkandarasi sawa na asilimia 40.6. Mkandarasi anahimizwa na kusimamiwa kwa karibu kuhakikisha kasi ya ujenzi inaongezeka na kazi,"anasema.

### USHIRIKI WA WAZAWA

Anasema kwa upande wa mkandarasi utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bandari ya Karema umeshirikisha wazawa kwa asilimia kubwa, kuanzia eneo la uongozi kada za mafundi na wafanyakazi wa kutwa.

"Kwa ujumla mkandarasi ameajiri idadi ya wafanyakazi 300 katika kada mbalimbali. Pia bidhaa za ujenzi kama kokoto, saruji, mchanga, nondo, udongo pamoja na vipuri vya mitambo ya ujenzi vinanunuliwa ama vinazalishwa hapa hapa nchini Tanzania,"anasema.

### VIKWAZO VILIVYOPO

Gasaya anaeleza kumekuwa na changamoto mbalimbali, ikiwapo mlipuko wa ugonjwa wa Uviko-19 uliosababisha kuchelewa baadhi ya vifaa vya ujenzi wa kazi za kudumu za bandarini Karema.

Anasema kwa sasa vifaa vimefika na mkandarasi anasisitiza kuongeza kasi ya ujenzi ili kufidia muda uliopotea na kumaliza mradi kwa wakati.

Meneja huyo anafafanua kuongezeka kina cha maji katika Ziwa Tanganyika, kulisababisha changamoto katika kazi ya kuandaa eneo la ujenzi wa miundombinu ya kudumu. Hata hivyo, anasema kazi kubwa ilifanyika kuhakikisha ufukiaji unafanyika, ili kupata eneo la kujenga miundombinu husika.

| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(11,995)** | **(2,604)** | **(14,531)** | **(4,938)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(11,995)** | **(2,604)** | **(14,531)** | **(4,938)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 57 | 60 | 57 | 60 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (599) | (130) | (726) | (247) |
| 15 | Mapato kwa Hisa zilizochujwa | (599) | (130) | (726) | (247) |
| 16 | **Idadi ya Matawi** | 4 | 5 | 4 | 5 |
| | ***BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI*** | | | | |
| 1 | Uwiano wa Faida kabla ya kodi na Wastani wa mali | -68.78% | -15.67% | -21.06% | -14.86% |
| 2 | Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -198.15% | -45.11% | -61.36% | -30.12% |
| 3 | Uwiano wa matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 124.15% | 77.23% | 111.94% | 76.73% |
| 4 | Uwiano wa mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali zinazozalisha | 6.77% | 7.43% | 6.19% | 5.54% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA WA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31.12.2021 | 30.09.2021 | 31.12.2021 | 31.12.2020 |
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (11,991) | (1,009) | (14,515) | (5,062) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 11,283 | 683 | 12,434 | 4,353 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 535 | (431) | 617 | 10,896 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 5,709 | (6,304) | 6,677 | (16,437) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 256 | (202) | (9) | 2,237 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (554) | (1,208) | (1,860) | (5,605) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (4) | (12) | (16) | - |
| | -SMR | 16 | (385) | (46) | 1,691 |
| | - Mengineyo | - | - | (36) | 1,346 |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | ***5,251*** | ***(8,868)*** | ***3,246*** | ***(6,580)*** |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (28) | (24) | (896) | (108) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | | | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (7,416) | (1,589) | (6,267) | 817 |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(7,444)** | **(1,613)** | **(7,163)** | **709** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 8,008 | 2,734 | 11,777 | 8,915 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **8,008** | **2,734** | **11,777** | **8,915** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **5,815** | **(7,747)** | **7,861** | **3,044** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka/Mwaka | 10,799 | 18,546 | 8,753 | 10,424 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka/Mwaka | **16,614** | **10,799** | **16,614** | **13,468** |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

Saini:

**SANJEEV ANAND**
Ofisa Mtendaji Mkuu
Tarehe: 26 Januari 2022

**GEORGE MSAMBAZI**
Mkuu wa Fedha
Tarehe: 26 Januari 2022

**JOHN MWAKASONDA**
Mkaguzi Mkuu wa Ndani
Tarehe: 26 Januari 2022

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi.

Saini:

**VISWANATHAN SUNDARAM**
Mjumbe wa Bodi
Tarehe: 26 Januari 2022

**HASHIMAH BINTI ISMAIL**
Mjumbe wa Bodi
Tarehe: 26 Januari 2022

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2021

| Mwaka wa sasa | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2021** | **28,940** | | **(11,320)** | **7,455** | | **-** | **25,076** |
| Marekebisho ya mwaka uliopita | | | (36) | - | | | **(36)** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (14,531) | | | | **(14,531)** |
| | | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | 4,451 | (4,451) | | | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | | | |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| Nyongeza ya Mtaji | 11,777 | | | | | | 11,777 |
| **Salio la mwisho wa kipindi 31.12.2021** | **40,717** | **-** | **(21,437)** | **3,005** | **-** | **-** | **22,286** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2020** | **20,025** | | **(4,086)** | **4,140** | | **-** | **20,079** |
| Marekebisho ya mwaka uliopita | | | (109) | | | | (109) |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (3,809) | | | | (3,809) |
| | | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | (3,315) | 3,315 | | | |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | | | |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| Nyongeza ya Mtaji | 8,915 | | | | | | 8,915 |
| **Salio la mwisho wa kipindi 31.12.2020** | **28,940** | | **(11,320)** | **7,455** | | **-** | **25,076** |

# HABARI ZANZIBAR



ICB
INTERNATIONAL COMMERCIAL BANK

## TARIFFS GUIDE - 2021

DISCLOSURE MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATION, 2014

MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES

| Type of Charge | Item / Transaction | TZS | USD | EURO | GBP |
|---|---|---|---|---|---|
| Minimum Opening Balance | ICB Savings Account | 20,000 | 50 | 50 | 50 |
| | ICB Salary Account | - | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Chuo (Students) Account | 2,000 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Wazee ( Senior Citizen) Account | Free | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Current Account -Personal | 50,000 | 50 | 50 | 50 |
| | ICB Premier Current Account | 1,000,000 | 500 | 500 | 500 |
| | ICB Premier Savings Account | 1,000,000 | 500 | 500 | 500 |
| | ICB Current Account - Corporate | 100,000 | 100 | 100 | 100 |
| | ICB Lenga (Goal ) Account | 20,000 | 100 | 100 | 100 |
| | ICB Kikundi ( Group ) Account | 50,000 | N/A | N/A | N/A |
| | Al-Wadiyah Savings Accounts | 20,000 | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Maintenance Fee | ICB Savings Account | 2,000 | 1.5 | 1.5 | 1.5 |
| | ICB Salary Account | 2,000 | N/A | N/A | N/A |
| | Al-Wadiyah Savings Account | Free | Free | Free | Free |
| | ICB Lenga (Goal ) Account | Free | Free | Free | Free |
| | ICB Kikundi ( Group ) Account | Free | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Wazee (Senior Citizen) Account | Free | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Premier Savings Account | 20,000 | 10 | 15 | 15 |
| | ICB Chuo (Students) Account | Free | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Premier Current Account | 20,000 | 10 | 15 | 15 |
| | ICB Current Account - Corporate | 15,000 | 7 | 7 | 7 |
| | ICB Current Account -Personal | 10,000 | 5 | 5 | 5 |
| Minimum Operating Balance | ICB Savings Account | 5,000 | 100 | 100 | 100 |
| | ICB Salary Account | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Chuo (Students) Account | - | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Wazee ( Senior Citizen) Account | - | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Current Account -Personal | 50,000 | 0 | 0 | 0 |
| | ICB Premier Current Account | 1,000,000 | 500 | 500 | 500 |
| | ICB Premier Savings Account | 500,000 | 500 | 500 | 500 |
| | ICB Current Account - Corporate | 50,000 | 0 | 0 | 0 |
| | ICB Lenga (Goal ) Account | 20,000 | 100 | 100 | 100 |
| | ICB Kikundi ( Group ) Account | 50,000 | N/A | N/A | N/A |
| | Al-Wadiyah Savings Accounts | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| Extra Charge on Transaction below Minimum Balance | ICB Savings Account | 600 | 1.2 | 1.2 | 1.2 |
| | ICB Salary Account | 600 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Chuo (Students) Account | N/A | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Wazee ( Senior Citizen) Account | N/A | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Staff Savings Account | N/A | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Current Account -Personal | 600 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Premier Current Account | 5,000 | 1.2 | 1.2 | 1.2 |
| | ICB Premier Savings Account | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Current Account - Corporate | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Lenga (Goal ) Account | 2,000 | N/A | N/A | N/A |
| | Al-Wadiyah Savings Accounts | N/A | N/A | N/A | N/A |
| Cash Withdrawal Fees | Cash withdraw at the counter (All Current accounts): Daily limits | Up to TZS 5Mil - 2000 , Above TZS 5Mil charge 0.13% Max TZS120,000 | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount |
| | Cash withdraw at the counter (All Savings accounts except ICB Chuo and Lenga Account): Daily limits | Up to TZS 5Mil - 1500 , Above TZS 5Mil charge 0.13% Max TZS 170,000 | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount |
| | premature withdrawal and withdrawal more than 1 time per quarter ( ICB Recurring Account & ICB Lenga Account respectively) | 2% charge of the principal amount | 2% charge of the principal amount | 2% charge of the principal amount | 2% charge of the principal amount |
| Fund Transfers / Remittances | Internal Transfers within ICB Bank | Free | Free | Free | Free |
| | Cross border transfers (TT, SWIFT) - outward | N/A | Up to USD50,000.00 charge is USD50 | | |
| | Cross border transfers (TT, SWIFT) - outward | N/A | above USD50,000.00 charge is USD75 | | |
| | Inward Transfers (TT, SWIFT) | Free | USD 15 | | |
| | Amendment of TISS, SWIFT Message | 11,800 | USD 11.8 | | |
| | Amendment of TT, SWIFT Message | N/A | USD 20 | | |
| | TISS | 11,800 | USD 11.8 | | |
| | EFT (Bulk Payments): Out&Inward/salary processing fee | 3,000 per transaction | USD 2 per transaction | | |
| | Stop Payments (TISS/EFT/SWIFT) | 20,000 | USD 20 | | |
| Cash Deposit | ICB Accounts | Free | Free | Free | Free |
| | ICB Agency Banking | Free | N/A | N/A | N/A |
| | Bulk Cash | Free | Free | Free | Free |
| | Deposit of Coins | 0.1% of the Amount | N/A | N/A | N/A |
| | Small Denomination (1, 5, 10, and 20) | N/A | 5% of the Amount | 5% of the Amount | 5% of the Amount |
| Balance Enquiry / Statement | ICB ATM Balance Enquiry | 300 | N/A | N/A | N/A |
| | Balance Enquiry - POS | 300 | N/A | N/A | N/A |
| | Balance Enquiry Within Banking Hall | Free | Free | Free | Free |
| | ICB Internet Banking | Free | Free | Free | Free |
| | ICB Agency Banking | 500 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Mobile (APP) | Free | Free | Free | Free |
| | interim statement | 1000 per page | 1 per page | 1 per page | 1 per page |
| | Monthly statement & E-statement | Free | Free | Free | Free |
| Cheque Deposit | Cheque From other Banks | Free | Free | Free | Free |
| | Outward Special Clearance – Local Settlement | 53,100 | 52.8 | 46 | 39.5 |
| | Inward Clearing | 1,000 | 1 | 1 | 1 |
| | Inward /Outward cheque return ( technical reason) | 10,000 | 10 | 10 | 10 |
| | Inward /Outward cheque return ( insuffient fund) | 50,000 | 20 | 20 | 20 |
| Cheque Book | Cheque Book 100 Leaves | 100,000 | 50 | 50 | 50 |
| | Cheque Book 50 Leaves | 50,000 | 25 | 25 | 25 |
| | Stop payment order per leaf; Reported Lost/Stolen Cheque Book/leaf (per notice) | 35,000 | 23.6 | 17.7 | 17.7 |
| Bankers Cheque | Commission per issued Cheque | 30,000 | 23.6 | 17.7 | 17.7 |
| | Cancellation of Banker's cheque | 30,000 | 23.6 | 17.7 | 17.7 |
| Standing Instruction | SI - Set up/Amendment/closure | Free | Free | Free | Free |
| | SI-Execution per Entry within ICB | Free | Free | Free | Free |
| | SI-Execution per Entry outside ICB | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| | Unpaid SI due to Insufficient funds | Free | Free | Free | Free |
| ATM /DEBIT CARDS | **ATM Card issuance fee** | | | | |
| | ICB Master Debit Card | 15,000 | 7 | 7 | 7 |
| | ICB Virtual Master Card | 3,400 | 1 | 1 | 1 |
| | Umoja Switch Card | 11,800 | N/A | N/A | N/A |
| | **ATM Card replacement fee** | | | | |
| | ICB Master Debit Card | 16,000 | 7 | 7 | 7 |
| | ICB Virtual Master Card | 3,500 | 1 | 1 | 1 |
| | Umoja Switch Card | 11,800 | N/A | N/A | N/A |
| | **Annual Card Maintenance** | | | | |
| | ICB Master Debit Card | 9,500 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Virtual Master Card | 35,000 | N/A | N/A | N/A |
| | Umoja Switch Card | 11,800 | N/A | N/A | N/A |
| | **ATM Transaction fee** | | | | |
| | ATM card activation | Free | | | |
| | Blocking/Hotting ATM card | Free | | | |
| | Umoja ATM Cash Withdrawal | 1,300 | N/A | N/A | N/A |
| | Umoja ATM Interbank Fund Transfer | 1,300 | N/A | N/A | N/A |
| | Umoja ATM Intrabank Fund Transfer | 1,300 | N/A | N/A | N/A |
| | Umoja ATM Transfers to Card-Less - (Remmitances) | 1,300 | N/A | N/A | N/A |
| | Umoja ATM Balance Inquiry | 300 | N/A | N/A | N/A |
| | Umoja ATM Mini Statement | 300 | N/A | N/A | N/A |
| | POS Withdrawal up to TZS 20,000,000 | 2,000 | N/A | N/A | N/A |
| | ATM Cash Withdrawal fee per transaction Mastercard local | 4,000 | Local trn < USD15 0.5%: Local trn >USD15 - 1.1% : Cross- border 1.6% | | |
| | ATM Cash Withdrawal fee per transaction Mastercard International | 8,000 | | | |
| Internet / Mobile Banking | Registration | Free | Free | | |
| | Monthly Service Fee (Corporate) | 15,000 | USD 8 | | |
| | Monthly Service Fee (Personal) | 7,000 | USD 4 | | |
| | Funds Transfer between Selcom managed banks | TZS 500 | | | |
| | Funds Transfer from Bank account to agents | TZS 500 | | | |
| | NHC payments | TZS 1,000 | | | |
| | Selcom Card funds transfers | TZS 500 | | | |
| | TANESCO Postpaid Electricity Bill payment | Free | | | |
| | TFDA- Certification application fee payment | TZS 1,000 | | | |
| | Transfers through ICB Internet Banking | TZS 1,000 | | | |
| | Transfers through Internet Banking File Upload Within | TZS 500 | | | |
| | Transfers through Internet Banking File Upload TISS | TZS 5,000 | | | |
| | Transfers through Internet Banking File Upload EFT | TZS 1,000 | | | |
| | Transfers through Internet Banking File Upload B2W | TZS 500 | | | |
| | UTT investor payments | TZS 1,000 | | | |
| | DSTV Payments | | | | |
| | 1 - 200,000/- | TZS 1,000 | | | |
| | 200,000.01 to 500,000 | TZS 2,000 | | | |
| | 500,000.01 + | TZS 5,000 | | | |
| General Account Operations | Confirmation of Balance and Audit Statement | 50,000 | 25 | 25 | 25 |
| | Salary processing manually per entry | 500 | N/A | N/A | N/A |
| | Salary and Bulk payments outside the Bank | 3,000/transaction plus transfer fee | N/A | N/A | N/A |
| | Advisory service - charged per advice | 2,500 | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS |
| | Vouchers - Information less than one year | 15,000 | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS |
| | Salary Alert per message | 118 | N/A | N/A | N/A |
| | Court Order Closing of Account | Free | Free | Free | Free |
| | Deliberate closing of Corporate account | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| | Deliberate closing of Personal account | 11,800 | 5 | 5 | 5 |
| | **Cash Change** | | | | |
| | Cash Coins per bag of TZS 100,000 | 1,180 | N/A | N/A | N/A |
| Bonds & Guarantee | Issuance of Bid Bond - Cash cover | 0.5% per Quarter | | | |
| | Issuance of Bid Bond - Other Security | 1.42% Per Quarter | | | |
| | Perfomance Bond-Cash Cover | 0.5% per Quarter | | | |
| | Perfomance Bond-Other security | 1.42% Per Quarter | | | |
| | Extentions | 1.42% Per Quarter | | | |
| | Amendments | Simple amendments$50 | | | |
| | Cancellations of Returned guarantees | Free | | | |
| | Cancellations of guarantees if not Returned | 20000 | | | |
| Advanced Payment Guarantee | Issuance - Cash cover | 0.5% Min 100,000 | | | |
| | Issuance - Security | 1.42% Min100,000 | | | |
| | **Import Collections (IC)-Inward Foreign Doc & Bills for Collections** | | | | |
| | Handling Commissions | 0.5% Min usd 100 | | | |
| | Correspondance swift charges | Usd 50 | | | |
| | **Export Collections (EC)-Outwar Foreign Doc & Bills for Collections** | | | | |
| | Handling Commissions | 0.5% Min usd 100 | | | |
| | Correspondance Commission-per tracer | Usd 50 | | | |
| | Courier Charges | Usd 100 | | | |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

**Name:**

| | | |
|---|---|---|
| Sanjeev Anand | Chief Executive Officer | 26.01.2022 |
| George Msambazi | Head of Finance | 26.01.2022 |
| John Mwakasonda | Head of Internal Audit | 26.01.2022 |

# Rais Mwinyi ataka taasisi za bima imara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ili nchi za kiafrika ziweze kutekeleza vyema mageuzi ya kiuchumi na kukuza ustawi wa wananchi ni lazima kuwa na sekta na taasisi za bima zilizo imara na zenye kwenda sambamba na kasi ya maendeleo ya Sayansi na Teknolojia katika karne ya 21.

Dk. Mwinyi alisema hayo katika ufunguzi wa Mkutano wa Bima kwa nchi za Afrika, uliofanyika katika Hoteli ya Madinat Bahr, iliyopo Mbweni jijini Zanzibar.

Alisema katika kujenga na kuendeleza uchumi wa kisasa, uwapo wa mfumo, sheria na taratibu madhubuti za uendeshaji wa shughuli za bima ni muhimu ili kuwapa wawekezaji imani na uhakika wa usalama wa mitaji wanayotaka kuwekeza.

Alisema pamoja na kuwapo maendeleo, Afrika inapaswa kuendelea kuimarisha sekta hiyo ili kuyafikia makundi yote ya wananchi yanayojishughulisha na shughuli za kiuchumi, hususan katika sehemu za vijijini. Alisema wananchi wengi wamekuwa wakiendesha shughuli zao bila kuwa na kinga ya bima na kutoa wito kwa mataifa ya Afrika kuwaelimisha wananchi wao umuhimu wa kuwa na bima na zitolewe kwa gharama nafuu na kwa wakati muafaka, hususan wananchi wanapopata misukosuko ya kiuchumi.

Rais Dk. Mwinyi alielezea furaha aliyonayo kutokana na maudhui ya mkutano huo yanayosisitiza umuhimu wa kuongeza juhudi katika kufikisha huduma za bima kwa wananchi wengi zaidi ili kukuza sekta hiyo ikiwamo Bima ya Afya, Bima ya Maisha, pamoja na kuwajengea uwezo watendaji.

Alisema Serikali ya Zanzibar inalenga kuanzisha Bima ya Afya, ikiwa ni hatua ya kuimarisha utoaji wa huduma hizo kwa wananchi, kwa kipindi kirefu ilishindwa kukidhi haja kutokana na kutegemea bajeti yake kwa asilimia 100.

Alizialika kampuni za Bima Barani Afrika kuwekeza Zanzibar ili kuendeleza uchumi wa Buluu, akibainisha kuwapo fursa nyingi za kiuchumi.

"Hatutopenda wawekezaji tunaowavutia kuja kuwekeza Zanzibar kwenye Bandari za kisasa, kwenye uvuvi, kwenye mafuta na gesi, wanakata bima zao nje, ni vyema tukahakikisha wanakata hapa hapa nchini," alisema. Dk. Mwinyi aliwahakikishia washiriki wa mkutano huo, kuwa Serikali ya Zanzibar itaendelea kushirikiana na Kampuni za Bima barani Afrika ili kuhakikisha malengo ya kufikisha huduma bora za bima kwa wananchi wote mjini na vijijini zinafikiwa.

Naye, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Jamal Kassim Ali, alisema ni wakati muafaka kwa washiriki wa mkutano huo kujadili umuhimu wa shughuli za Bima ya Afya Barani Afrika, kuambatana na azimio la Abuja (Abuja Declaration).

Katibu Mkuu wizara hiyo, Dk. Malik Akil, alisema serikali inaamini kuna kazi kubwa inayopaswa kufanyika ili kuhami rasilimali za bahari na zile zenye nasaba na hizo ili kuiwezesha Zanzibar kufikia azma ya kuimarisha uchumi wa buluu.

Kwa upande wake, Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Khadija Issa Said, alisema pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika uendeshaji wa sekta ya Bima Afrika na hususan Tanzania, kuna changamoto zinazoikabili sekta hiyo, ikiwamo uelewa mdogo wa wananchi, hasa walio vijijini.

# Mahakimu watakiwa kutoa dhamana inapostahili

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKIMU Kisiwani Pemba wametakiwa kutoa dhamana kwa washtakiwa wanaostahiki kupewa kwa mujibu wa makosa yao ili kupunguza msongamano katika Magereza.

Kaimu Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Shaaban, alisema hayo wakati alipofanya ziara kwenye mahakama za Pemba kuona utendaji wa majukumu pamoja na magereza yaliyopo Kangagani na Tundauwa kisiwani humo.

Aliwataka mahakimu kufanya uchunguzi wa kina na kujiridhisha kabla ya kutoa dhamana hatua ambayo itasaidia kupunguza msongamano wa watuhumiwa magerezani ikiwamo watoto.

Aliwataka watendaji wa Magereza kuhakikisha watoto hawachangamani na watuhumiwa watu wazima ili kuepuka matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia katika magereza.

"Nawaagiza mahakimu kutoa dhamana kwa watuhumiwa wanaostahiki kupewa dhamana ili kupunguza msongamano katika magereza na watoto wanatakiwa kutenganishwa na watu wazima kuepuka matukio ya udhalilishaji wa kijinsia," alisema.

Alisema Mahakama Kuu ya Zanzibar imejipanga kufanya kazi kwa kuzingatia weledi pamoja na kasi ya kusikiliza mashauri ya wananchi yanayofikishwa mbele ya vyombo vya sheria ili kuona haki inatendeka.

Aliyataja mafanikio ya Mahakama Kuu kuwa ni kusikiliza kesi za udhalilishaji wa kijinsia kwa kasi na kutoa huduma zake kwa watuhumiwa.

"Tumejipanga kuongeza kasi ya kusikiliza kesi za udhalilishaji wa kijinsia kwa watuhumiwa ambapo kwa wananchi wanatakiwa kutoa ushirikiano ikiwamo ushahidi," alisema.

Naye Jaji Mkazi Pemba, Ibrahim Mzee, alisema ameanza mchakato wa kuzifuatilia kesi zote zilizokatiwa rufani kwa ajili ya kusikilizwa.

"Nimeanza kuzipitia kesi zote zilizokatiwa rufani Mahakama Kuu kwa ajili ya kusikilizwa na kuona zile zinazostahiki kufikishwa katika ngazi hiyo na kuanza kutajwa," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa mdhamini wa Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Pemba, Halima Khamis Haji, alisema wamefurahishwa na kuwapo kwa Jaji mkazi Pemba hatua itakayoongeza kasi ya kusikiliza kesi za rufani za watuhumiwa mbalimbali zinazoletwa katika ngazi hiyo.

"Tumefurahishwa na ujio wa jaji mkazi kisiwani Pemba ambapo ni moja ya kilio cha muda mrefu cha wananchi pamoja na watuhumiwa kuwapo kwa kiongozi wa aina hiyo atakayesikiliza rufaa zinazowasilishwa na watuhumiwa kwa haraka," alisema.

HABARI MICHEZO

# KIBADENI ATAKA VIONGOZI SIMBA WACHUKUE HATUA

**Na Saada Akida**

MCHEZAJI na kocha wa zamani wa Simba, Abdallah Kibadeni amewataka viongozi kukaa na wachezaji wao kwa ajili ya mahojiano na kupata ufumbuzi katika kipindi kigumu wanachokipitia cha kupoteza mechi mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kibadeni alisema amepata bahati ya kuona mechi zote za Simba na kuwataka viongozi kuchukuwa hatua za haraka kukaa na wachezaji kwa ajili ya kuzungumza nao.

Alisema amefanikiwa kuona mechi zote ambazo Simba zinapoteza, lakini akiangalia timu yake hiyo ya zamani inatawala kila idara na kucheza vizuri huku ikishindwa kutumia nafasi wanazotengeneza.

"Tatizo linaloonekana hapa ni ushambuliaji, kwa sababu hata mechi dhidi ya Kagera Sugar tumekosa nafasi nyingi, jambo hili linatakiwa kufanyiwa kazi haraka hasa viongozi kukaa na wachezaji kuzungumza nao kuona shida iko wapi," alisema.

"Ukiangalia washambuliaji wetu ni wazuri zaidi ya wapinzani wetu tunaocheza nao, lakini wanashindwa kufunga, hali hii ikiendelea hatuwezi kutetea ubingwa wetu," alisema Kibadeni.

Alisema hana wasiwasi na kocha mkuu, Pablo Franco kwa sababu timu inacheza vizuri na kutawala kila idara wapinzani, tatizo ni wafungaji.

Hata hivyo, Kibadeni alisema mashabiki wasikate tamaa na waendelea kuisapoti timu yao na ana imani viongozi wa Simba kufanyia kazi hali wanayopitia kwa sasa.

Wakati huo huo Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Simba, Ahmed Ally, amewaomba mashabiki kushikamana katika kipindi kigumu wanachopitia.

Alisema matokeo wanayoyapata sio mazuri, lakini yasiwatoe katika mipango yao na kushikamana zaidi.



Kikundi cha Ngoma za Asili, Wanne Star, kikitoa burudani wakati wa hafla ya utoaji wa tuzo za Kiswahili ya Mabati – Cornell ya Fasihi ya Afrika iliyoandaliwa na Kampuni ya Mabati ya Alaf jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbeya City yajifungia kuisoma Yanga

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mbeya City umesema unatumia wiki ya kombe la Shirikisho kujiimarisha kila idara ikiwamo safu ya ulinzi kwa ajili ya kuivaa Yanga kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mbeya City iliondolewa katika hatua ya makundi na African Sports kwa mikwaju ya penalti 4-3, baada ya suluhu ya dakika 90.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, alisema hawako katika michezo ya kombe la shirikisho, hivyo wanatumia muda huu kuwasoma Yanga.

Alisema msimu huu amedhamiria kuchafua watu, wakati akiwasoma Yanga katika michezo ya Kombe la Shirikisho pia atafanyia kazi mapungufu ya kikosi chake kujiimarisha zaidi katika safu yake ya ulinzi na ushambuliaji.

"Hatukufanikiwa kusonga mbele katika michuano ya Kombe la Shirikisho, sasa tunatumia nafasi hii kujiimarisha kuelekea mechi yetu dhidi ya Yanga kuhakikisha nao tunawachafua kama ilivyokuwa kwa Simba," alisema Lule.

Aidha, alisema ana imani utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa na mgumu na msimu huu amedhamiria kuweka historia ya kuzifunga timu hizo na kumaliza ligi katika nafasi ya juu.

"Yanga watakuwa nyumbani, hilo halitatufanya kuhofia kwa sababu tumekuwa tukiwasoma ubora na madhaifu yao nina imani kipindi wao wanacheza FA, tunatumia kujiimarisha zaidi," aliongeza.

Mbeya City watarajiwa kuingia jijini Dar es Salaam Februari Mosi, kwa ajili ya mchezo dhidi ya Yanga utakaopigwa Februari 5, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

# Azam FC vs Transit Camp kwenye FA leo

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Azam FC, Abdihamid Moallin, amesema wamejipanga vizuri kwenye mchezo wao wa leo wa Kombe la Shirikisho dhidi ya Transit Camp katika hatua ya 32 utakaopigwa katika Uwanja wa Azam Complex.

Moallin alisema, itakuwa mechi ya kwanza tangu asaini mkataba wa miaka mitatu kurithi mikoba ya George Lwandamina.

Kocha huyo alisema ana imani na kikosi chake kufanya vizuri katika michezo iliyoko mbele yao ikiwamo dhidi ya Transit Camp ili kusonga mbele katika michuano hiyo.

"Tumefanyia kazi mapungufu yaliyotoke katika michezo iliyopita ya ligi, tunaenda kucheza shirikisho, tutakuwa na utofauti kwenye mbinu na namna ya kucheza ili tuweze kupata ushindi," alisema Moallin.

Alisema ameona mabadiliko makubwa katika timu hiyo na anatarajia wachezaji wake kufanya vizuri katika mchezo huo na iliyoko mbele yao kwa lengo la kufikia kinachotarajiwa kutwaa ubingwa wa michuano hiyo.

# Manara aiondoa Yanga Princess kwenye ubingwa

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imekiri kuwa ni vigumu sana kwa timu yao ya wanawake Yanga Princess kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara msimu huu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, msemaji wa klabu hiyo Haji Manara amesema kwa jinsi Ligi Kuu ya Wanawake msimu huu inavyokwenda ni wazi kubwa ubingwa kwao ni mgumu kwani wameachwa pointi nyingi na vinara, lakini kikosi chao kinatakiwa kifanyiwe maboresho na hii haiwezi kuwa msimu huu.

"Unajua mimi siyo kama wale wanaosema eti Yanga haiwezi kuwa mabingwa wa soka la wanaume Tanzania kwa sababu wanakata pumzi, tutawakuta njiani, hapana kwenye ukweli lazima niseme, huku kwenye soka la wanawake kwa jinsi ligi inavyokwenda ni ngumu sana kutwaa ubingwa kutokana na jinsi kikosi chetu kilivyo na wenzetu walivyojipanga, niseme tu kikosi chetu kinatakiwa kifanyiwe maboresho kadhaa, kwa hiyo ikitokea sawa, lakini ukweli lazima tuseme kwa upande huo wa wanawake msimu huu ni vigumu," alisema Manara.

## ZISIKUPITE

### MULLER AWANIWA
MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich na Ujerumani, Thomas Muller amezivutia Newcastle United na Everton, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 akikaribia mwaka wa mwisho wa mkataba wake na timu hiyo ya Ligi Kuu England, Bundesliga. ***(Sportbild - via Star)***

### BARCA WAKOMAA NA HAALAND
BARCELONA wanafanyia kazi mpango wa kuchangisha euro milioni 100 kufadhili usajili wa mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 21 msimu huu.***(Goal)***

### BRIGHTON WAIKATALIA NEWCASTLE
KLABU ya Brighton imekataa ofa kutoka kwa Newcastle kwa ajili ya mlinzi wa England, Dan Burn mwenye umri wa miaka 29. ***(Athletic)***

### BRUNO AITAKA NEWCASTLE
KIUNGO wa kati wa Lyon, Bruno Guimaraes ameiambia klabu hiyo kuwa anataka kuhamia Newcastle, ambayo imewasilisha ofa mezani kwa Mbrazili huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(L'Equipe)***

### LAMPARD HUYO EVERTON
FRANK Lampard kwa sasa ndiye anayeongoza kuwania nafasi ya kuwa kocha mpya wa Everton. ***(Independent)***

### BROJA KUJIUNGA SOUTHAMPTON
KLABU ya Southampton inatayarisha dau litakaloweka rekodi klabuni hapo la pauni milioni 25 ili kumpa Armando Broja mkataba wa kudumu baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Albania mwenye umri wa miaka 20 kujiunga na klabu hiyo kutoka Chelsea kwa mkopo wa msimu mmoja mwanzoni mwa msimu. ***(Fabrizio Romano)***

### BAKKER ATAKIWA NEWCASTLE
NEWCASTLE imeanza tena mazungumzo ya kumsajili mlinzi wa Uholanzi, Mitchel Bakker kutoka Bayer Leverkusen, huku klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, ikiwa na nia ya kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 katika dirisha hili la Januari. ***(90 min)***

### SPURS KUMTOA NDOMBELE
KLABU ya Tottenham Hotspur imekubali kumtoa kwa mkopo kiungo wa kati wa Ufaransa, Tanguy Ndombele mwenye umri wa miaka 25 kwenda Valencia. (Telefoot)

### TRAORE ATAKIWA BARCA
WINGA wa Wolves raia wa Hispania anayelengwa na Tottenham Hotspur, Adama Traore mwenye umri wa miaka 26, sasa anatazamwa kama chaguo kwa Barcelona ikiwa wanaweza kupata dili la kumuuza mshambuliaji wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24. ***(ESPN)***

### DYBALA AWINDWA LIVERPOOL
LIVERPOOL wamefanya mawasiliano na mshambuliaji wa Juventus na Argentina, Paulo Dybala, huku mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 ukikamilika msimu wa joto. ***(TuttoMercato - via Sun)***

### PHILLIPS AGOMBEWA
MLINZI wa Liverpool, Nat Phillips mwenye umri wa miaka 24, anawindwa na Newcastle, West Ham na Watford. ***(Independent)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LEWANDOWSKI KUBAKIZWA BAYERN KWA NAMNA YOYOTE

Ofisa Mtendaji wa klabu abainisha hawawezi kumwachia kirahisi, kwani ni mchezaji muhimu kwao na...

**MUNICH, Ujerumani**

BAYERN Munich itafanya "kila kitu" kumbakiza Robert Lewandowski kwa "muda mrefu kadiri inavyowezekana", lakini Niklas Sule anapanga kuondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu.

Mkataba wa sasa wa Lewandowski unamalizika mwishoni mwa msimu 2022-23 na kumekuwa na ripoti kwamba Bayern wanaweza kumuacha mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland kuondoka akiwa huru ili kutoa nafasi kwa nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 ambaye ameshinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Fifa ikiwa ni kwa mara ya pili, mabao yake 34 kwenye mashindano yote msimu huu yanamfanya kuongoza kwa mabao 10 zaidi kuliko mchezaji yoyote katika ligi kubwa tano za Ulaya.

Afisa Mtendaji wa Bayern, Oliver Kahn amebainisha Jumatano kwamba, mabingwa hao wa Bundesliga hawana mpango wa kumuachia Lewandowski aondoke.

"Kwa uhakika kabisa yeye ni mchezaji wa kiwango cha juu," alisema Kahn akiwaambia waandishi wa habari.

"Sio tu kwa mabao ambayo anafunga mara kwa mara, lakini kwa kiwango ambacho amekuwa akicheza kwa miaka kadhaa.

"Bila shaka tutajaribu kumbakiza Robert. Yeye ni kama hakikisho letu, kwa namna anavyocheza soka. Tutafanya kila kitu tunachoweza kumbakiza Robert kwa muda mrefu na sisi."

Hata hivyo, mlinzi wa kati Sule mwenye umri wa miaka 26 ataondoka hapo kwenye dimba la Allianz Arena baada ya kukataa kuongeza mkataba mpya.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 878

MECHI KALI
NANTES
VERSUS
BREST
1 | 2.13
X | 3.25
2 | 3.35

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KIVUMBI ROBO FAINALI AFCON



**YAOUNDE, Cameroon**

MICHUANO ya Mataifa ya Africa (AFCON), imeingia kwenye hatua ya robo fainali na mchezo wa kwanza utapigwa Jumamosi ya Januari 29.

Mchezo huo wa kwanza utawakutanisha Gambia dhidi ya wenyeji Cameroon ambapo kipute cheke kitapigwa kwenye dimba la Douala.

Gambia ilitinga katika hatua hiyo baada ya kuitoa Guinea kwenye hatua ya 16 bora kwa ushindi wa bao 1-0.

Wao Cameroon wametinga hatua hiyo baada ya ushindi wa 2-1 dhidi ya Comoros na wakajihakikishia nafasi ya kucheza robo fainali.

Mechi nyingine itazikutanisha Burkina Faso dhidi ya Tunisia mchezo utakaopigwa kwenye uwanja wa Garoua.

Burkina Faso walitinga hatua hiyo baada ya kuwafunga Gabon kwa penalti 7-6 baada ya muda wa kawaida na ziada kumalizika kwa sare ya 1-2, huku Tunisia wakiwatoa Nigeria kwa ushindi wa bao 1-0.

Jumapili Misri watacheza na Morocco kwenye uwanja wa Ahmadou Ahidjo, wakati Senegal watawavaa Equatorial Guinea kwenye uwanja wa Douala.

Fainali ya michuano hiyo itapigwa Februari 6, mwaka huu.

# Martial afunguka kuondoka Man United

**SEVILLE, Hispania**

ANTHONY Martial ameelezea sababu ya kuondoka Manchester United kwa mkopo kwani anataka "kufurahia tena soka".

Sevilla ilitangaza kumsajili kwa mkopo mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa Jumanne, ambapo Martial atacheza kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, hadi mwishoni mwa msimu huu.

Wakati kiasi cha fedha hakujatajwa kwenye dili hilo, iliripotiwa kwamba, Sevilla iliwagharimu kiasi cha euro milioni 6 ikijumuishwa kwenye mshahara wa Martial na ada ya uhamisho wa mkopo.

Mkurugenzi wa michezo wa Sevilla, Monchi alithibitisha kwamba ililazimika Martial akubali kupunguziwa mshahara ili kuweza kutua hapo.

Kocha wa muda wa United, Ralf Rangnick alibainisha mwezi uliopita kwamba, Martial alitaka kuachwa kwenye timu hiyo kwa sababu ya kukosa nafasi ya kuanza kikosi cha kwanza.

Lakini sasa Martial mwenyewe amewekа wazi kuwa kuondoka kwake ni sababu alitaka kufurahia tena soka.

"Kwa upande wangu mimi ilikuwa kuhusu nia ya kutaka tena kufurahia soka," alisema Martial akiiambia tovuti ya Sevilla.

"Ilikuwa ni hisia nzuri kuungana na kocha (Julen Lopetegui), na niliamua kwamba, ulikuwa wakati muafaka mimi kuja Sevilla.

"Nilizungumza na yeye (Lopetegui) mara chache, na alionyesha nia ya kinitaka mimi kuja kucheza hapa."



## HABARI MICHEZO


,152,880

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 29/01/22 | 18:00 | Amorebieta vs Girona | 2.80 | 3.09 | 2.50 |
| 02. 29/01/22 | 18:00 | Tranmere vs Forest Green | 2.64 | 3.18 | 2.59 |
| 03. 29/01/22 | 18:00 | Oldham vs Rochdale | 2.80 | 3.25 | 2.41 |
| 04. 29/01/22 | 18:15 | Nancy vs Amiens | 2.52 | 3.16 | 2.77 |
| 05. 29/01/22 | 23:00 | Real Oviedo vs Almeria | 2.75 | 3.09 | 2.55 |
| 06. 29/01/22 | 23:00 | SBV Excelsior vs Emmen | 2.56 | 3.49 | 2.46 |
| 07. 30/01/22 | 16:30 | Vicenza vs Alessandria | 2.66 | 3.05 | 2.66 |
| 08. 30/01/22 | 18:30 | FC Sion vs Grasshoppers | 2.56 | 3.40 | 2.56 |
| 09. 30/01/22 | 18:30 | FC Vizela vs Vitoria Guimaraes | 2.90 | 3.20 | 2.47 |
| 10. 30/01/22 | 19:00 | Cardiff vs Nottingham | 2.55 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 30/01/22 | 20:30 | PAOK vs Olympiakos | 2.61 | 3.10 | 2.71 |
| 12. 30/01/22 | 23:00 | Lens vs Monaco | 2.77 | 3.26 | 2.46 |
| 13. 30/01/22 | 23:00 | Ponferradina vs Tenerife | 2.42 | 3.11 | 2.91 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 28/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:15 | 5169 | Persepam MU vs Psis Semarang | 2.84 | 3.08 | 2.36 |
| 14:30 | 2591 | Cagliari Youth vs Roma Youth | 3.67 | 3.96 | 1.74 |
| 14:30 | 4671 | US Lecce youth vs Sampdoria Youth | 2.79 | 3.51 | 2.19 |
| 16:00 | 2353 | Marines FC Gisenyi vs Kiyovu Sports | 3.79 | 3.07 | 1.96 |
| 16:00 | 3020 | El Fahem vs Hapoel Petah Tikva | 2.05 | 3.16 | 3.75 |
| 16:00 | 3322 | Barito Putera vs PSM Makassar | 3.08 | 3.22 | 2.15 |
| 16:00 | 3333 | Hilal Al-Quds vs Shabab AL Khaleel | 4.99 | 4.03 | 1.54 |
| 16:00 | 3334 | Thagafi Tulkarem vs Islami Qalqilya | 2.12 | 3.18 | 3.18 |
| 16:00 | 4175 | Hapoel Kfar Saba vs Bnei Yehuda | 2.42 | 3.02 | 3.07 |
| 16:00 | 4678 | Charlton U23 vs QPR U23 | 1.86 | 3.81 | 3.33 |
| 16:00 | 5576 | Forest Rangers vs Power Dynamos | 2.50 | 2.79 | 2.93 |
| 16:30 | 1054 | Fiorentina Youth vs Bologna Youth | 1.64 | 4.30 | 4.70 |
| 16:45 | 4917 | Arema vs Persipura Jayapura | 1.46 | 4.40 | 7.00 |
| 17:00 | 1309 | Jamshedpur vs FC Goa | 1.84 | 3.47 | 3.71 |
| 17:00 | 5143 | Swansea U23 vs Colchester U23 | 1.66 | 4.20 | 4.60 |
| 18:00 | 2579 | Nea Salamis vs Onisilos Sotira FC | 1.43 | 4.14 | 6.36 |
| 18:30 | 4042 | Sassuolo Youth vs Pescara Youth | 1.25 | 5.58 | 8.27 |
| 20:00 | 1600 | Paeek vs Pafos FC | 4.46 | 3.72 | 1.73 |
| 20:00 | 2467 | Istra vs HNK Gorica | 3.03 | 3.27 | 2.15 |
| 21:00 | 1640 | Dunkerque vs Paris FC | 3.64 | 3.24 | 2.01 |
| 21:00 | 2881 | Villefranche Sur Saone vs Sete 34 FC | 1.45 | 4.00 | 6.83 |
| 21:00 | 4441 | AC Ajaccio vs AJ Auxerre | 2.09 | 3.19 | 3.48 |
| 21:00 | 5373 | Boulogne vs Red Star | 2.74 | 2.99 | 2.59 |
| 21:00 | 5377 | Kickers Wurzburg vs Freiburg II | 2.52 | 3.26 | 2.66 |
| 21:00 | 5591 | Sepsi Osk vs Universitatea Craiova | 2.59 | 2.98 | 2.79 |
| 21:00 | 5593 | Nimes vs Valenciennes | 2.22 | 3.10 | 3.25 |
| 21:00 | 5660 | Caen vs Niort | 2.00 | 3.19 | 3.73 |
| 21:00 | 5848 | Sporting Farense vs CF Estrela | 2.13 | 3.43 | 3.08 |
| 21:30 | 2416 | CD Serverense vs CD Binisalem | 5.00 | 3.80 | 1.68 |
| 22:00 | 1430 | Lommel United vs KFC Oosterzonen | 2.10 | 3.75 | 2.93 |
| 22:00 | 2437 | FC Oss vs Den Bosch | 1.82 | 3.62 | 3.86 |
| 22:15 | 4928 | FC Aarau vs Neuchatel Xamax | 1.99 | 3.47 | 3.23 |
| 22:30 | 1592 | Airbus UK Broughton vs Conwy Borough | 1.20 | 5.60 | 11.59 |
| 22:30 | 2277 | Ammanford vs Goytre United | 6.16 | 3.94 | 1.46 |
| 22:30 | 4539 | Ruthin Town vs Llandudno FC | 2.51 | 3.09 | 2.65 |
| 22:30 | 4924 | Risca United vs Llantwit Major | 6.55 | 4.62 | 1.37 |
| 22:45 | 1933 | Morton vs Raith Rovers | 2.98 | 3.18 | 2.30 |
| 22:45 | 3456 | Haverfordwest vs Penybont | 3.76 | 3.71 | 1.77 |
| 22:45 | 3906 | Bala Town vs Newtown AFC | 2.74 | 3.32 | 2.30 |
| 22:45 | 4090 | Huddersfield vs Stoke City | 2.49 | 3.13 | 2.79 |
| 22:45 | 4829 | Ballymena Utd vs Cliftonville Belfast | 3.66 | 3.37 | 1.89 |
| 22:45 | 4997 | Caernarfon Town vs The New Saints | 8.49 | 5.60 | 1.24 |
| 22:45 | 5723 | St Truiden vs Charleroi | 2.95 | 3.04 | 2.46 |
| 23:00 | 1327 | Aberystwyth Town vs Cefn Druids | 1.28 | 5.20 | 7.89 |
| 23:00 | 2465 | Nantes vs Brest | 2.13 | 3.25 | 3.35 |
| 23:00 | 4340 | Valladolid vs Sporting Gijon | 1.57 | 3.83 | 5.50 |
| 23:00 | 5347 | CD Buzanada vs CD Marino | 2.75 | 3.40 | 2.50 |
| 23:00 | 5916 | Lija Athletic vs Naxxar Lions | 3.15 | 3.80 | 2.08 |
| 23:15 | 3936 | CD Trofense vs Benfica Lisbon B | 2.97 | 3.31 | 2.24 |
| 23:30 | 4374 | Alverca Futebol vs Sporting Lisbon B | 1.98 | 3.60 | 3.60 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# SURE BOY AHOFII NAMBA YANGA

**Na Dennis Fussi**

LICHA ya kiungo wa mpya wa Yanga, Salum Abubakary 'Sure Boy' kutopata nafasi ya kuanza kikosi cha kwanza mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini hilo halimpi presha.

Sure Boy amesema kuwa hana presha ya nafasi ya kuanza kikosi cha kwanza sababu anajua muda ukifika atacheza na kuisaidia timu yake kutimiza malengo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Sure Boy amesema kuwapo na ushindani na namba kwenye timu hiyo hakumpi presha sababu hata timu aliyotoka Azam ilikuwa hivyo, lakini bado aliendelea kucheza kikosi cha kwanza.

"Ushindani kwenye mpira ni kitu cha kawaida kwa mchezaji na bidii yako ndio inapaswa ifanye kazi kwa hiyo nipo tayari kwa ushindani ingawa kwenye timu mimi bado mgeni lazima nikae nje ili niangalie wenzangu wanavyocheza," amesema Sure Boy.

Kiungo huyo mwenye uwezo mkubwa wa kumiliki na kuichezesha timu amejiunga na Yanga kwenye dirisha dogo msimu huu akiwa mchezaji huru baada ya kuvunja mkataba wake na Azam.




Mbunifu wa Mavazi Mary Fernandez (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu shindano la Lady in Red Fashion Show lililoandaliwa na kampuni ya Hugo Domingo, linalotarajiwa kufanyika Februari 12, mwaka huu, jijini humo, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Siku ya Wapendanao ambayo husherehekewa kila Februari 14. Kushoto ni Harith Juma kutoka Hugo Domingo na jaji wa shindano hilo, Didas Katona. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Namungo yaitisha Mtibwa

**Na Dennis Fussi**

KOCHA Msaidizi wa Namungo, Jamhuri Kihwelo 'Julio' ametamba kuifunga Mtibwa Sugar katika mchezo wa Ligi Kuu utakaopigwa Febuari 6 uwanja wa Ilulu mjini Lindi.

Julio amesema wachezaji wao tayari wameanza kuwaelewa kitu gani walimu wanataka ndio maana hawajapoteza mchezo kwenye mechi mbili za ligi walizocheza ugenini siku za karibuni.

"Tumekwenda Moshi tukatoka sare ya bila kufungana na Polisi na tukawafunga Coastal Union bao 3-1 kwao kwa hiyo tupo vizuri na hata hao Mtibwa wajiandae kwa kichapo hapa Ilulu hatoki mtu salama," amesema Julio.

Kocha huyo amesema nia ni kuhakikisha wanashinda kila mechi watakayocheza kwenye uwanja wa Ilulu na kutoa kipigo kuanzia mabao 2 kwenda mbele na hilo linawezekana kutokana na ubora wa kikosi cha Namungo.

Michezo

Ijumaa Januari 28, 2022

Nipashe

UKURASA 21



Lewandowski kubakizwa Bayern kwa namna yoyote



Kocha wa Yanga, Nesreddine Nabi, akilakiwa na mashabiki wakati kikosi hicho kilipotua jana Mwanza tayari kwa maandalizi ya mchezo wao wa Kombe la Shirikisho dhidi ya Mbao FC, utakaopigwa Jumamosi kwenye uwanja wa CCM Kirumba. **PICHA: YANGA**

# KIIZA: NILIWAZIDI AKILI MABEKI WA SIMBA SC

## ●●●Asema aliwatoroka, akatumia uzoefu kujiweka sehemu sahihi na kufunga, huku akiwasifia kwamba...

**Na Adam Fungamwango**

MFUNGAJI wa bao pekee kwenye mechi ya kiporo ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Kagera Sugar dhidi ya Simba, Hamisi Kiiza, amesema ulikuwa ni ujanja wake pamoja na uzoefu kuwatoroka mabeki wa timu hiyo na kukaa eneo sahihi kabla ya kufunga.

Pia ameomba radhi kwa viongozi, wapenzi na mashabiki wa Kagera kwa kulimwa kadi nyekundu kwenye mchezo huo.

Kiiza, mchezaji aliyewahi kuichezea Yanga mwaka 2011 hadi 2015, kabla ya kujiunga na Simba mwaka 2015 hadi 2016 amesema ilikuwa ni umakini wake, lakini wapinzani wao wana mabeki wazuri na wazoefu tofauti na watu wanavyodai.

"Mabeki wa Simba ni wazuri na wazoefu, ila ni umakini wangu, nikawatoroka na nikakaa sehemu sahihi nikafunga, huu ni uzoefu na ujanja wangu, lakini mabeki wo ni wazuri sana," alisema mchezaji huyo raia wa Uganda.

Alisema kuwa alijiandaa kuonyesha kitu tofauti kwenye mechi hiyo ili jina lake lirudi tena kwenye midomo ya mashabiki, kwani wapo wanaomfahamu, lakini wamemsahau, na wapo ambao wakati anachezea timu hizo walikuwa wadogo na hawamjui.

"Nilikuwa nataka kuweka heshima kwenye jina langu, wengi wamenisahau na hawajui kama nipo, lakini wengine wakati nacheza soka Tanzania walikuwa wadogo," alisema. Kuhusu kutolewa nje kwa kadi nyekundu, Kiiza alisema kuwa hiyo ndiyo mara ya kwanza tangu kuanza kucheza soka.

"Maishani mwangu sijawahi kupata kadi nyekundu, nawaomba radhi viongozi, wachezaji wa wapenzi wa timu ya Kagera Sugar kwa kile nilichokifanya, lakini kikubwa ni kwamba tumepata ushindi," alisema.

Straika huyo alifunga bao dakika ya 70 lililoipa ushindi wa 1-0 Kagera kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera na kuwafanya wanachama na mashabiki wa Simba wakiwa hawaamini kilichotokea, huku viongozi wote pamoja na Kocha Mkuu, Pablo Franco akikataa kuzungumza na waandishi wa habari.

Hata hivyo, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ahmed Ally ameomba radhi kwa waandishi wa habari, wanachama na mashabiki wa Simba na wadau wa soka kwa ujumla kutokana na kadhia hiyo.

Pia amewaomba radhi wanachama na mashabiki wa Simba kutokana na matokeo mabaya na kipindi kigumu ambacho timu inapitia kwa sasa.

Pamoja na kufungwa Simba inaendelea kushika nafasi ya pili kwa kusalia na pointi 25, lakini ikiwa imezidiwa pointi 10 na vinara Yanga, Kagera Sugar ikitoka nafasi ya 11 hadi ya tisa ikiwa na pointi 16.

# Nabi amwandaa Ushindi kuiua Mbao FC

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Yanga, Nesreddine Nabi amesema amemwandaa winga wake, Chiko Ushindi kuwa fiti kwa lengo la kumpa majukumu kwenye mchezo wa Kombe la Shirikisho dhidi ya Mbao FC, Jumamosi.

Yanga itacheza na Mbao Jumamosi hii katika uwanja wa CCM Kirumba na Ushindi aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo akitarajiwa kuwa miongoni mwa wachezaji watakaoanza kwenye mchezo huo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Nabi alisema maandalizi yanaendelea vizuri na wanafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mchezo uliopita na kuimarisha ubora wao.

Alisema ana imani hakuna mechi ambayo itakuwa rahisi kwao kwa sababu timu yoyote inapokuwa katika mashindano hujiandaa vizuri na ana imani Mbao itawapa ushindani mkubwa.

"Hii ni mechi ngumu na ya ushindani ukiangalia anayepoteza hapa anatolewa na akishinda anasonga mbele, tunahitaji kwenda kutafuta matokeo mazuri tunalazimika kujiandaa vizuri kuelekea mchezo wetu huo," alisema kocha huyo.

Alisema anatarajia kufanya mabadiliko ya kikosia na inategemea na siku moja kabla ya maandalizi ya mchezo huo na ana imani kuna wachezaji atawapa nafasi ambao hawakucheza katika hizi mechi zilizopita.

Nabi alisema kuhusu Ushindi ni mzuri na ana imani muda sio mrefu ataonekana katika baadhi ya mechi baada ya nyota kuwa fiti kwa kiwango anachokihitaji.

Alisema nyota huyo alikuwa na programu maalum kwa ajili ya kumjenga kimwili na kumrejesha katika kiwango bora na kuweza kufanya vizuri atakapopewa nafasi.

"Ushindi amesajiliwa kwenye kikosi cha Yanga kutokana na uwezo wa kutumia miguu yote miwili jambo ambalo ni nadra kwa wachezaji wengi wanaocheza nafasi ya winga," alisema Nabi.

Alisema hakuna urahisi, lakini wakipambana na wachezaji watakapokuwa watulivu kwa kila idara ana imani kubwa ya kufiti kinachotarajiwa na mashabiki wao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >